BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 4. | Mhe. Shaaban Ali Othman | - | Jimbo la Mpendae |
| 5. | Mhe. Hemed Suleiman Abdulla | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 6. | Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman (OR) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu. |
| 7. | Mhe. Masoud Ali Mohammed (OR) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole. |
| 8. | Mhe. Haroun Ali Suleiman (OR) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora/Jimbo la Makunduchi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | Mhe. (OR) | Jamal Kassim Ali | - | MBM/Waziri wa Nchi, Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni. |
| 10. | Mhe. | Dkt Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge. |
| 11. | Mhe. | Dkt. Soud Nahoda Hassan | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje |
| 12. | Mhe. na | Simai Mohammed Said | - | MBM/Waziri wa Elimu Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu |
| 13. | Mhe. | Tabia Maulid Mwita | - | MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais |
| 14. | Mhe. na | Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Ardhi Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake |
| 15. | Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake |
| 16. | Mhe. | Suleiman Masoud Makame | - | MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga |
| 17. | Mhe. wa | Abdulla Hussein Kombo | - | MBM/Waziri wa Uchumi Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18. Mhe. | Lela Muhamed Mussa | - | MBM/Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake |
| 19. Mhe. | Abdalla Abasi Wadi | - | Jimbo la Nungwi |
| 20. Mhe. | Ali Abdulgulam Hussein | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 21. Mhe. | Ali Suleiman Ameir | - | Jimbo la Pangawe |
| 22. Mhe. | Ameir Abdalla Ameir | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 23. Mhe. | Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 24. Mhe. | Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 25. Mhe. | Azza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 26. Mhe. | Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 27. Mhe. | Bakar Hamad Bakar | - | Jimbo la Wawi |
| 28. Mhe. | Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |
| 29. Mhe. | Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) | | Nafasi za Wanawake |
| 30. Mhe. | Habibu Ali Muhamed | - | Jimbo la Mtambwe |
| 31. Mhe. | Haji Omar Kheri | - | Jimbo la Tumbatu |
| 32. Mhe. | Haji Shaaban Waziri | - | Jimbo la Uzini |
| 33. Mhe. | Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Kwamtipura |
| 34. Mhe. | Harusi Said Suleiman | - | Jimbo la Wete |
| 35. Mhe. | Hassan Hamad Omar | - | Jimbo la Kojani |
| 36. Mhe. | Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 37. Mhe. | Hudhaima Mbarak Tahir | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. | Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 39. Mhe. | Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |
| 40. Mhe. | Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 41. Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | Jimbo la Chwaka |
| 42. Mhe. | Kombo Mwinyi Shehe | - | Jimbo la Wingwi |
| 43. Mhe. | Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 44. Mhe. | Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 45. Mhe. | Mihayo Juma Suleiman | - | Jimbo la Mwera |
| 46. Mhe. | Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 47. Mhe. | Mohamed Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 48. Mhe. | Mohamed Ahmada Salum | - | Jimbo la Malindi |
| 49. Mhe. | Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bumbwini |

| | | |
|---|---|---|
| 50. Mhe. Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 51. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 52. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 53. Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 54. Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 55. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 56. Mhe. Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 57. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | - | Uteuzi wa Rais |
| 58. Mhe. Omar Said Shaaban | - | Uteuzi wa Rais |
| 59. Mhe. Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 60. Mhe. Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 61. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 62. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |
| 63. Mhe. Saidi Saleh Salim | - | Jimbo la Tumbe |
| 64. 5Mhe. Sabiha Filfil Thani | - | Nafasi za Wanawake |
| 65. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |
| 66. Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 67. Mhe. Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |
| 68. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | - | Jimbo la Kiembe Samaki |
| 69. Mhe. Sulubu Kidongo Amour | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 70. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Nafasi za Wanawake |
| 71. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Jimbo la Micheweni |
| 72. Mhe. Shaib Hassan Kaduara | - | Jimbo la Chake Chake |
| 73. Mhe. Yahya Rashid Abdulla | - | Jimbo la Kwahani |
| 74. Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 75. Mhe. Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 76. Mhe. Zawadi Amour Nassor | - | Jimbo la Konde |

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

**Kikao cha Kumi – Tarehe 25 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi cha tarehe 15 Februari, 2021 Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir aliuliza swali la nyongeza linalotokana na swali la msingi Nam. 67 na katika kikao cha tarehe 17 Februari, 2021 Mhe. Asha Abdalla Mussa aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 23 na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali aliahidi kujibu maswali hayo kwa maandishi.

Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali asome majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Wajumbe hao. Ahsanteni Waheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Salma Mussa Bilal swali lake la nyongeza ambalo niliahidi kulijibu kwa maandishi kama ifuatavyo:-

(a) Je, ni kesi ngapi za wanafunzi ambao wamedhalilishwa zilizofikishwa katika Vituo vya Polisi kutoka mwaka 2016 hadi 2020.

(b) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa.

**(a) IDADI YA KESI ZILIZOFUATILIWA TOKEA MWAKA 2017- 2020**

| MWAKA | NDOA | UJAUZITO | UBAKAJI NA ULAWITI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 2016-2017 | 25 | 26 | 21 | 72 |
| 2017-2018 | 16 | 22 | 30 | 68 |
| 2018-2019 | 8 | 17 | 18 | 43 |
| 2019-2020 | 13 | 55 | 27 | 95 |
| **JUMLA** | **62** | **120** | **96** | **278** |

Aidha, kwa mwaka 2016/2017 jumla ya kesi 241 hazikuripotiwa ambapo kesi za ndoa 61 ziligundulika, kesi 74 za ujauzito na kesi 106 za udhalilishaji kupitia uhakiki tulioufanya kujua hali halisi ya takwimu ya mambo hayo.

(b) Kuhusu hatua za ziada ambazo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inazichukua ni kama ifuatavyo:-

1. Kufukuzwa kwa wanafunzi ambao wamefunga ndoa.

2. Kunyang’anywa leseni ya ualimu kwa mwalimu ambaye atahusika na kesi yoyote kati ya hizo iwe ujauzito au ubakaji na ulawiti kwa mujibu wa Kanuni na Miiko na Maaadili ya Kazi ya Ualimu ya mwaka 1996 inavyoeleza, kifungu cha 7 “mwalimu atakayethibitika kuvunja au kukiuka miiko na maadili ya kazi ya ualimu usajili wake utafutwa, kunyang’anywa leseni ya kusomesha na kupoteza kazi yake kwa mujibu wa sheria”. Aidha, kesi hizo za walimu husimamiwa na Mwanasheria wa Wizara. Ahsante sana Mhe. Spika.

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani juu ya Hotuba ya Mgawanyo wa Rasilimali Fedha kufuatia Mabadiliko ya Muundo wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti):** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani juu ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mgawanyo wa Rasilimali Fedha, kufuatilia Mabadiliko ya Muundo wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 59**

**Changamoto Kubwa ya Ajira kwa Vijana Wanaomaliza Masomo**

**Mhe. Habib Ali Mohamed** - Aliuliza:-

Ajira ni haki ya kila mtu mwenye sifa kulingana na nafasi husika lakini imeonekana kwamba utekelezaji wake dhana hiyo uko tofauti.

Je, serikali ina mpango gani wa kuajiri vijana wenye sifa ambao wamemaliza masomo yao.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora -** Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Habib Ali Mohamed swali lake Nam. 59 kama ifuatavyo:

Kwanza, napenda kukubaliana na Mhe. Habib Ali Mohamed ya kwamba ajira ni haki ya kila Mzanzibari mwenye sifa kulingana na nafasi ya kazi husika iliyotangazwa. Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini imekuwa ikifanya hivyo kwa kuzingatia kifungu 57 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni ya 7 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.

Mhe. Spika, kutokana na malengo hayo, serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini tayari imeajiri vijana wengi wenye sifa na viwango vya elimu tofauti ikiwemo Astashahada, Stashahada na Shahada na itaendelea kufanya hivyo kwa mujibu wa mahitaji na kwa kuzingatia Mpango wa Rasilimali Watu wa kila Wizara na Taasisi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Tume ya Utumishi Serikalini ilipanga kuajiri vijana 5,657 katika wizara na idara mbali mbali Unguja na Pemba ambapo hadi kufikia

mwezi Disemba, 2020 Tume ya Utumishi Serikalini ilifanikiwa kuajiri vijana 3,280 sawa na asilimia 57. Tume ya Utumishi Serikalini itaendelea kuajiri vijana hao waliosalia mara tu serikali itakapojiridhisha kuwepo kwa haja hiyo ya kuajiri kwa mujibu wa mahitaji.

**Mhe. Habib Ali Mohamed**: Nashukuru Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa hivi karibuni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika hotuba zake nyingi tulikuwa tunamsikia kwamba ataondoa ukabila na ubaguzi katika maeneo yote.

Je, Mhe. Waziri atatuhakikishia vipi kwamba katika masuala ya kuajiri hakutakuwa na itikadi ya kisiasa.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Spika, Sera ya Chama cha Mapinduzi na Sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuondosha ubaguzi wa aina zote na kamwe hatutokaribisha suala zima la ubaguzi kwa njia yoyote ile, iwe kwa jimbo, mkoa au kisiwa. Sisi tunachukulia kwamba Wazanzibari wote ni wamoja chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tupo pamoja na tunashirikiana kwa pamoja wala hatobaguliwa mtu kwa urefu wake wala ufupi wake. *(Makofi)*

**Nam. 61**

**Maslahi Madogo kwa Watendaji**

**Mhe. Habib Ali Mohamed** - Aliuliza:-

Wafanyakazi ambao wanasafisha barabara wengi wao ni wanawake wanaonekana wakifanya kazi ngumu lakini wanapata maslahi madogo.

Je, serikali imejipangaje katika kuboresha maslahi ya wafyagiaji wa barabarani.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Habib Ali Mohamed swali lake Nam. 61 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba wasafishaji wengi katika maeneo ya barabara ni wanawake, hali hii inatokana na ongezeko kubwa la idadi ya wafanyakazi wa kada ya uhudumu (usafishaji) kuwa ni wanawake.

Hivyo, katika kukabiliana na chamgamoto hii, Baraza la Manispaa Mjini limebinafsisha huduma ya usafishaji wa taka kwa Kampuni ya *Green Waste Pro* katika maeneo ya Kusini, Magharibi na Mji Mkongwe ambapo ilianza kazi rasmi tarehe 15/12/2020 na eneo lililobakia ni upande wa Kaskazini ambalo litahudumiwa na Baraza la Manispaa kwa kutumia wafanyakazi wake wa ndani. Vile vile, Baraza katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi hao limejipanga kutekeleza yafuatayo:-

1. Kuwapatia vifaa vya kinga ikiwemo barakoa, *gloves*, sare na viatu.

2. Kuboresha maslahi ya wafanyakazi hao ikiwemo kupima afya angalau kwa mwaka mara moja.
3. Kuwapatia posho la mazingira magumu wafanyakazi hao.

Aidha, lengo la kuboresha hali ya wafanyakazi hawa wasafishaji sio kwa Manispaa ya Mjini peke yake, bali ni Mabaraza yote, Halmashauri na Manispaa zote za Unguja na Pemba.

**Mhe. Habib Ali Mohamed:** Nakushukuru Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, swali langu la nyongeza kama ifuatavyo. Kwanza nampongeza kwa majibu mazuri aliyonipa.

Mhe. Spika, hivi karibuni Wilaya ya Chake Chake kulikuwa na kampuni binafsi ambayo ilikuwa ikishughulikia suala la usafishaji katika Baraza la Mji Wilaya ya Chake Chake. Je, ni sababu zipi zilizopelekea kuvunjwa mkataba ule.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Habib Ali Mohamed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sababu kuu zilizopelekea kuvunja mkataba ule ni kuona kwamba hauna tija kwetu sisi kama Baraza la Mji Chake Chake. *(Makofi)*

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa majibu yake.

Mhe. Spika, baada hii kampuni kupewa kazi na matangazo yaliyotoka ni kwamba hizi nyumba ziwe zinaweka taka katika vipolo wakati wanakwenda kupeleka katika majaa. Katika mtazamo wa muda mfupi ni sahihi kwa sababu hivyo vipolo vinapatikana majumbani. Lakini katika mtazamo wa muda mrefu hivyo vipolo vitatoweka.

Serikali ina mkakati gani kuweza kurahisisha utupaji wa taka kutoka kwa wananchi na kupeleka sehemu ambapo hizi taka zitazolewa bila ya kuwa na hivyo vipolo wala vitu vyengine vya kuwekea. Nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, mpango wa serikali tuliokuwa nao ni kuhakikisha kwamba utupaji au uondoaji wa taka katika maeneo ambayo yanawekwa na wananchi. Moja ni kuhakikisha kwamba baada ya kutoka kwenye mfumo huu wa kutumia vipolo ambavyo kama ulivyoeleza ni mpango wa kupita kwa sasa. Lengo letu ni kutengeneza utaratibu ambao katika Manispaa, Mabaraza na hizo Halmashauri kunakuwa na *point of collection* ambazo zitakuwa karibu na maeneo ya wananchi kuwaelekeza kwamba kuwepo kwa *dust bin* zitakazokuwa zinasimamiwa na Mabaraza, Halmashauri au Manispaa ambazo zitatoka kwa wananchi na kwenda kupelekwa katika *collection point* ambazo zitakwenda kwenye majaa yetu makuu. *(Makofi)*

**Mhe. Yahya Rashid Abdulla:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Swali langu mimi ni dogo tu kwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Spika, hii kampuni ambayo ameitaja ya *Green Waste Pro* wanaifuatilia vipi mikataba ya vijana wetu ambao wanaajiriwa na hiyo kampuni. Kwa sababu kuna malalamiko mengi sana katika suala zima la mikataba ya vijana wanaotumika katika kampuni hiyo. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Yahya Rashid Abdulla swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kimsingi, tunaifuatilia kampuni ile na mkataba ambao tumeuingia kati ya Manispaa na Kampuni ile ya *Green Waste Pro* ni wa miaka miwili. Moja ya eneo ambalo tumewataka basi ni zaidi ya asilimia 90 ya vijana ambao watawachukua wawe ni vijana ambao ni wazalendo kwa maana ni vijana wetu ambao wanatoka katika mazingira yetu.

Mhe. Spika, katika hili tumewataka wahakikishe kwamba vijana hawa:

1. Wanapata malipo yaliyoelekezwa kwa mujibu wa sheria.

2. Wanafunguliwa akaunti zao au kwa maana wanapata malipo yao ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Lakini pia wanachukua jitihada za makusudi ili kuhakikisha kwamba wanapima afya zao na kuwapatia vitendea kazi. Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi.

Kwa hiyo, kimsingi ni kwamba tunawafuatilia na hatuiachi kampuni hii ifanye inavyotaka kwa sababu tunajua wanaofanya shughuli zile ni vijana ambao ni wetu sisi na ni wazalendo kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

**Nam. 75**

**Uwekwaji wa Taa za Kuongozea Gari Barabarani *(Traffic Light)***

**Mhe. Bakar Hamad Bakar** - Aliuliza:-

**Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ**

*(Mheshimiwa aliyeuliza swali hili ameliondoa)*

**Nam. 31**

**Serikali Kuwapatia Vyombo vya Uvuvi Wananchi Wanaojishughulisha na Uvuvi**

**Mhe. Hassan Hamad Omar -** Aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ni ya visiwa kwa kiasi kikubwa wananchi wake wanategemea shughuli za baharini kuendesha maisha yao kupitia uchumi wa buluu.

(a) Je, ni lini serikali itawasaidia wananachi kupata meli za uvuvi.
(b) Je, kwa nini serikali isielekeze nguvu zake katika kuboresha vyombo vya wavuvi wadogo wadogo ambao kimsingi ndio wanaosaidia kupatikana kwa ajira.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi -** Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar swali lake Nam. 31 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, katika kipindi cha miaka mitano (2021- 2025) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepanga kuagiza meli nne za uvuvi wa bahari kuu.

b) Mhe. Spika, serikali imeandaa mipango na utaratibu wa kuweka mazingira rafiki kwa wavuvi wadogo wadogo na wawekezaji wazalendo, ili kuwawezesha kufanya shughuli za uvuvi wa maji ya kina kirefu kwa ufanisi kwa kuwataka wavuvi kuendeleza vikundi ambayo vitaweza kuifikia mikopo kutoka taasisi za kifedha ambazo zimekubali kutoa mikopo nafuu.

Aidha, baadhi ya wawekezaji kutoka nje wameonesha nia ya kuingia mikataba na wavuvi wadogo wadogo kwa kuwapatia boti na nyenzo zote za uvuvi kwa makubaliano ya kuwataka samaki wote wanaovuliwa na wavuvi hao wawauzie wawekezaji hao kwa bei ya soko na kwa wakati huo huo kuwakata kidogo kidogo gharama za vifaa walivyopewa. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi naomba niulize swali la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa meli hizo nne hazikidhi haja kwa wavuvi walio wengi Zanzibar na wavuvi wetu kutokana na vyombo vyao hususan Wakojani chombo chao kimoja kinaingia watu 50 mpaka 60 na meli hizo zinazotegemewa hazifiki mabaharia 30 kuingia.

Je, huoni kuwa ni mpango wa kutuacha kwa walio wengi.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Tumesema kwamba meli nne ni meli ambazo zinaagizwa na serikali na ni mpango wa serikali, wapo wawekezaji binafsi wataleta meli za ziada. Kwa hivyo, meli ambazo zinaagizwa na serikali ni meli nne, lakini sio kwamba ni meli hizo nne tu ambazo zitaletwa nchini, zipo meli nyengine ambazo zitaletwa na wawekezaji binafsi. *(Makofi)*

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa Sekta ya Uvuvi kwa sasa inachangia zaidi ya asilimia 2.6 katika pato ghafi la uchumi wetu, lakini inatoa ajira ya moja kwa moja kwa watu wasiopungua laki mbili. Lakini kuna watu zaidi ya laki nne huitegemea sekta hii.

Je, Mhe. Waziri una mpango gani wa kutoa mafunzo kwa ajili ya kuwaandaa wavuvi wetu wadogo wadogo kuelekea katika kuimarisha hii sekta ya uchumi wa buluu kabla ya hata kuja hivyo vifaa ambavyo tunatarajia kwamba vitaweza kuwasaidia.

La pili, je, mpaka sasa hivi tuna idadi ya wavuvi wadogo wadogo wangapi katika takwimu yetu.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Swali la mwanzo la elimu Mhe. Spika, nafikiri nimekuwa nikilijibu mara nyingi sana suala hili, tunaendelea kutoa elimu na tutaendeea kutoa elimu na katika mipango yetu ya miaka mitano imo prgramu ya kutoa elimu kwa wavuvi wote. Swali la pili kwa sababu ni takwimu Mhe. Spika, naomba nilijibu kwa maandishi.

**Mhe. Haji Omar Kheri:** Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Najua kwamba Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kupitia ilani ya CCM aliahidi kununua meli na nyengine kuzileta Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa na mpango kupitia *ZAFICO* kununua meli nyengine za uvuvi. Je, hizi meli zitakazonunuliwa zinanunuliwa kupitia mfuko wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kama ni hivyo, meli hizi zitakuwa mali ya Zanzibar au zitakuwa ni mali ya *deep sea*.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Haji Omar Kheri swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, jana nilijibu swali hili kwamba meli hizi zinanunuliwa kutoka kwenye mfuko wa *IFAT*, kwa hiyo meli hizi zitakuwa ni mali ya Zanzibar pamoja na kwamba zimeagizwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, lakini kuna *portion* ya Zanzibar. Kwa hiyo, meli hizi zitakuwa mali ya Zanzibar. Swali lake la pili hebu nikumbushe tena.

**Mhe. Haji Omar Kheri:** Namshukuru kulizingatia swali la pili. Swali langu (a) lilikuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa na mpango wa kununua meli kupitia *ZAFICO*. Je, mpango huu ukoje.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Spika, meli ambayo ilikuwa inunuliwe na *ZAFICO actually* imeshanunuliwa bahati mbaya bado haijafika zilikuwa ni meli mbili. Meli ya kwanza ipo Zanzibar inafanya kazi, meli ya pili ilikuwa ifike tangu Januari haikuweza kufika kutokana na masuala ya *COVID-19*. Kwa hiyo, imeshanunuliwa na wakati wowote itafika Zanzibar.

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda niulize swali dogo la nyongeza. Je, Mhe. Waziri hizi meli nne zinazokuja tayari wataalam wa kuziendesha wameshapatikana isije kuwa zinakuja meli hapa siku mbili zinabuma.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi :** Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Suala la kusomesha mabaharia kwa ajili ya kuendesha meli hizo ni kwamba ni endelevu. Mhe. Spika, bado tunaendelea kufundisha vijana wetu katika suala la mabaharia na kama nilivyosema

kwamba tunajenga *university* ya kusomesha wavuvi na mabaharia katika mradi wetu tuliosaini hivi karibuni. Kwa hiyo, Mhe. Fatma nikuhakikishie suala hilo lipo akilini na tunaliendeleza vizuri sana.

**Mhe. Sulubu Kidongo Amour:** Ahsante Mhe. Spika, mimi nataka kumuuliza swali dogo tu la wavuvi kwa sababu jana nimeshindwa kukaa kwenye semina wavuvi jana wamenyang'anywa vifaa vyao vya uvuvi. Mhe. Waziri, ulitwambia kama kuna boti ambazo unazinunua kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo. Kwa nini unaanza kunyang'anya hivyo vifaa kabla hizo boti hujatoa.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, hatuna nia na wala hatutokuwa na nia ya kumnyang'anya mvuvi yeyote zana zake za uvuvi. Tunawanyang'anya wavuvi wanaotumia zana hizo kwa uvuvi haramu na hili ni suala la kisheria ambayo tumeipitisha wenyewe hapa. Kwa hiyo na jana nimeulizwa swali hilo Mhe. Spika, namna gani nitadhibiti uvuvi haramu, hii ndio namna yenyewe ambayo tunadhibiti uvuvi haramu.

**Nam. 29**

**Mikakati ya Kuwapatia Vijana Elimu katika Vyuo vya Amali**

**Mhe. Salma Mussa Bilal -** Aliuliza:-

Kwa dhati kabisa naomba niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga majengo katika maeneo mbali mbali ya Vyuo vya Amali nchini.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kuhakikisha lengo la kujenga vyuo hivyo linafikiwa na kuleta tija kwa vijana wetu.

(b) Kwa kuwa kuna vijana wetu wengi ambao wanafeli na kuzurura mitaani bila kazi. Je, serikali ina mikakati gani ya kuwapeleka vijana hao vyuoni huko ili kuwasaidia kupata elimu hiyo na kuweza kujiajiri badala ya kusubiri kupata ajira serikalini.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Lengo la kujenga Vyuo vya Mafunzo ya Amali nchini ni kuwapatia vijana taaluma ya ufundi unaoendana na soko la ajira ili waweze kujiajiri, kuajiriwa na kuwaajiri wengine ili kuepukana na utegemezi. Kwa kuhakikisha lengo hilo linafikiwa, serikali kupitia Wizara ya Elimu Mafunzo ya Amali imekuwa ikifanya juhudi mbali mbali kuhakikisha vijana wetu wanavutiwa na kujiunga na vyuo hivyo vya mafunzo ya amali. Miongoni mwa juhudi hizo ni kufanya tafiti ili kujua matakwa ya soko la ajira na kutoa mafunzo kwa vijana ya fani mbali mbali zinazoendana na matakwa ya soko hilo. Jumla ya fani 15 zinatolewa katika Vyuo vya Mafunzo ya Amali kwa sasa za muda mrefu na muda mfupi. Fani hizo ni Upishi, Huduma za Mahoteli, Useremala, Uunganishaji Vyuma, Ujenzi, Ufundi Bomba, Ufundi Umeme, *Electronics*, Ufundi

Mafriji na Viyoyozi, *ICT*, Kilimo, Uchoraji na Mapambo, Ufundi magari, Ufundi Umeme wa Magari na Ushoni.

Mhe. Spika, Wizara imeibua fani nyengine zenye ujuzi tofauti utakaowawezesha vijana kujiajiri kirahisi mara baada ya kuhitimu mafunzo hayo. Kwa mwaka huu wa fedha wa 2020/2021, Wizara kupitia Mamlaka ya Mafunzo ya Amali itaanza kufundisha fani mpya za uvuvi, ufundi wa zana za kilimo, ufugaji wa kuku wa mayai, pamoja ng'ombe na mbuzi wa maziwa, mafunzo ya kusindika vyakula *(spices*, mboga mboga, samaki na matunda), matumizi ya nishati mbadala, utunzaji wa bustani na mauwa, uchongaji wa vipuri, uungaji vifaa vya aluminium na ufundi wa vifaa vya uvuvi.

Aidha, serikali inawapatia mikopo isiyo na riba wahitimu wa Vyuo vya Mafunzo ya Amali wanaojiunga na vikundi kwa ajili ya kuendeleza ujuzi waliopatiwa katika vyuo kupitia fani walizosomea kwa lengo la kujiajiri na kupunguza umaskini.

(b) Serikali imeandaa Sera wezeshi ambayo inawapokea vijana waliohitimu elimu ya lazima na kujiunga na Mafunzo ya Amali. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa ikiwahamasisha vijana kujiunga na Vyuo vya Mafunzo ya Amali kupitia skuli, Masheha na Mabaraza ya Vijana.

Serikali pia imeweka ada ndogo kwa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Mafunzo ya Amali kwa mwaka ili vijana wengi waweze kujiunga na vyuo hivyo. Hadi sasa ada ya vyuo vya mafunzo ya amali kwa kijana ambaye anaishi nje ya dakhalia analipa 120,000/= kwa mwaka na 160,000/= kwa anayeishi ndani ya dakhalia.

**Mhe. Salma Mussa Bilal:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo amejibu lakini naomba nimuulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri, ulisema kwamba kuna fani 15 ambazo zinafundishwa za mwanzo katika vyuo vya amali. Nilikuwa nataka kujua kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020 ni vijana wangapi ambao wamejiunga na vyuo hivyo na wanawake ni wangapi na wanaume wangapi. Halafu pia nataka mchanganuo hasa ni fani ipi ambayo wamejiunga wanafunzi wangapi, wanawake wangapi na wanaume wangapi.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilal swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, mara nyingi mimi ninapokuja kujibu maswali huwa najitahidi kuwa na takwimu, lakini takwimu hizi amezitaka za undani kabisa na zenye mchanganuo tofauti kwa masomo na maeneo. Mhe. Spika, nitakuomba kwa swali hili nimpatie kwa maandishi ili aweze kuzifanyia kazi, ahsante sana.

**Mhe. Mtumwa Peya Yussuf:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Mhe. Waziri katika majibu yake alieleza kwamba vijana hawa wanapomaliza wanapewa mikopo nafuu kwa ajili ya kuendelea na shughuli zao. Nilikuwa nataka kujua katika mwaka 2019/2020 ni kiasi gani cha fedha kilichotolewa na kupewa mikopo vijana hawa. Na (b) ni vijana wangapi ambao walipatiwa mikopo hiyo. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mtumwa Peya Yussuf swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe.

Spika, suala la kutoa mikopo tunazingatia kutokana na fedha na uwezo ambao tunao. Lakini katika mwaka 2019/2020 tuliwatilia vikundi jumla kumi na tatu mikopo hiyo kwa upande wa Pemba na Unguja. Vikundi viwili kwa upande wa Pemba na kumi na moja kwa upande wa Unguja. Zaidi ya shilingi milioni 100 tulitoa kwa ajili ya mikopo hiyo, baadhi ya vikundi hivyo vimeshaanza kurudisha hiyo mikopo, kikundi kimoja kimeshamaliza kurejesha mkopo huo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kabla ya kuuliza swali naomba nichukue nafasi hii kuwaombea kila la kheri Klabu ya *Namungo FC* ya Lindi katika mashindano yao watakaocheza leo jioni. Mhe. Spika, pamoja na kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kumekuwa kuna *tendency* ya wanafunzi wengi ambao wanamaliza mafunzo ya vyuo vya amali uwezo wao kuwa mdogo katika kuhimili soko la ajira hasa kitaaluma. Je, sababu za msingi zinazopelekea uwezo wa wanafunzi hao kuwa mdogo ni mitaala ama ukosefu wa vifaa vya kujifunzia kwa maana kwamba vile vifaa vya kufanyia *practical* katika vyuo vyetu vya mafunzo ya amali.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Issa Haji Ussi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, suala la mitaala kwa upande wa *VTA* sisi ni chuo ambacho tumesajiliwa rasmi na tunatambulika na mitaala yetu ni mitaala ambayo kwa mujibu wa utaratibu na sheria tunazozifuata ni kwamba unaweza kufanya kazi kokote duniani. Kama ilivyo kawaida penye wengi pana mengi kwamba kila mmoja anategemea na juhudi katika elimu na uwezo wake mwenyewe binafsi ya kujituma. Sisi kwa takwimu tunazoziona na tunazozifanya kwamba vijana wetu wengi wanaingia katika soko la ajira. Tunazo changamoto katika lugha kwa wanafunzi ambao wanaingia katika maeneo mengine. Lakini kimsingi kwa mfano katika maeneo ya *electrical engineering* tulikuwa tuna changamoto katika mashine, lakini kwa sasa tayari tukiangalia takwimu zetu vijana wengi wameweza kuajiriwa katika masoko, hasa katika soko la utalii katika maeneo ya hoteli.

Wengi sasa hivi wamekuwa wanaingia katika fani, lakini mawazo yake labda kwa Mhe. Issa Haji Ussi anatukumbushia pia, labda kuna umuhimu wa kufanya utafiti, lakini utafiti tumefanya ndio maana mwanzo nilisema kwamba katika kozi ambazo tunazitaja mpya nilizungumzia kozi za ufundi wa kilimo, ufugaji wa kuku, *hospitality agro posing, mobile repair* na mengine. Haya yote yanatokana na baada ya utafiti kufanyika. Tuchukue mawazo yake na ushauri wa suala lake kwamba bado anahisi yeye kuna umuhimu zaidi. Kwa hiyo, mimi kama waziri mwenye dhamana nalichukua hili kulifanyia kazi.

**Nam. 41**

**Changamoto za Utaratibu wa Kuandikishwa Mtoto Skuli**

**Mhe. Hassan Hamad Omar -** Aliuliza:-

Ilielezwa kuwa ni wajibu wa mzazi kumpeleka mtoto skuli kupata haki ya elimu kwani mtoto ndiye kiongozi wa taifa la kesho.

(a) Kwa nini mtoto anapewa vikwazo kuandikishwa skuli, kufanya mitihani kwa kukosa cheti cha kuzaliwa wakati vyeti vina usumbufu kupatikana na ni jukumu la mzazi kuleta cheti na sio mtoto.

(b) Je, kwa nini mtoto anayekaa karibu na skuli anaweza kukosa nafasi ya kusoma lakini akapokelewa mtoto wa mbali

(c) Je, hatua gani zitachukuliwa kurekebisha hatua hiyo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 41 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Suala la kuandikishwa skuli kwa wanafunzi limewekewa utaratibu maalum ambao kila mzazi wa mwanafunzi anapaswa kuufuata. Miongoni mwa utaratibu huo ni mtoto kuwasilisha cheti chake cha kuzaliwa ili kuhakikisha taarifa zake ziko sahihi likiwemo jina lake, tarehe yake ya kuzaliwa, sehemu aliyozaliwa pamoja na taarifa za wazazi wake. Utaratibu huu husaidia sana kuweka kumbukumbu sahihi lakini pia kuondoa kasoro zinazoweza kujitokeza taarifa zake zitakapoandikwa kimakosa. Bado Wizara inawasisitiza wazazi wawatafutie watoto wao vyeti vya kuzaliwa na sio kutoa malalamiko watoto wao wanapotakiwa kuwasilisha taarifa zao za kuzaliwa. Mtoto anaandikishwa darasa la maandalizi akiwa na miaka minne kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2016. Muda huu unatosha kabisa kwa mzee kumtafutia mtoto wake cheti cha kuzaliwa kabla hajafikia umri wa kuandikishwa.

(b) Mhe. Spika, napenda kulijulisha Baraza lako tukufu kwamba utaratibu wa kuandikisha wanafunzi hauangalii umbali au ukaribu wa mtoto anapoishi au anapotoka. Kawaida watoto wote hupokelewa na kuandikishwa katika skuli ambayo mzee wake angependa mtoto wake asome.

(c) Wizara imejiridhisha kwamba bado hakuna changamoto kubwa zinazowakabili wazazi wakati wa kuwaandikisha skuli watoto wao. Hata hivyo, Wizara kabla ya kuandikisha watoto skuli hukutana na wazazi mbali mbali kupitia mikutano ya wazazi, wajumbe wa kamati ya wazazi na uongozi wa shehia, ili kujadili na kupeana miongozo ya uandikishaji wa wanafunzi. Utaratibu huu hufanyika kila mwaka na bado unaendelea.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake sahihi pamoja na hayo naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa kumekuwa na usumbufu wa kutosha wa kupatikana vyeti vya kuzaliwa na amesema kupatikana cheti cha kuzaliwa ni kuweka kumbukumbu sawa. Usumbufu huu utawasaidiaje wananchi, mtu anafika miaka mitano hajapata cheti za kuzaliwa cha mtoto, anafikia umri wa kwenda skuli bado hajapata cheti cha kuzaliwa. Je, Mhe. Waziri wizara yako itasaidia vipi wananchi kupata vyeti vya kuzaliwa.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan Hamad Omar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, kwanza naomba nitoe taarifa kwa Baraza lako tukufu kwamba serikali haina mpango wa

kuwanyima wananchi vyeti vyao vya kuzaliwa na ni utaratibu tumeweka serikali ambapo kila mwananchi anatakiwa afuate hivi vigezo kutokana na sifa ambazo mtoto anatoka katika eneo ili kuweka kumbukumbu sahihi za mtoto, lakini pia kuepukana na matatizo ambayo yanaweza kumfikia yule mtoto na kulinda haki za mtoto. Sasa mimi niseme katika kila maeneo sisi kwa upande wa serikali wizara zote mbili zinasimamia elimu ya msingi pamoja na elimu ya sekondari tuna maafisa wa elimu katika maeneo husika katika halmashauri zetu.

Nimuombe Mhe. Hassan Hamad Omara ikiwa kuna chochote jimboni kwake au eneo lake husika kuna changamoto ambayo anaitambua yeye kwa sababu yeye ndio mwakilishi wa wananchi basi atuletee orodha ya wananchi wake wenye malalamiko halafu sisi kwa upande wa serikali tutayafanyia kazi kwa mashirikiano. Nikiamini kwamba serikali inafanya kazi kwa mashirikiano ya pamoja. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 55**

**Kutokamilika kwa Visima vya Ras-al-Khaimah**

**Mhe. Machano Othman Said -** Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kutupa nguvu. Lakini pili, nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wa Zanzibar, Makamu wa Pili wa Rais, wewe Mhe. Spika na Kaimu Waziri wa Afya kwa kufuatilia afya yangu kuwa vizuri na namshukuru Mwenyezi Mungu sasa nipo salama. Niwashukuru pia Waheshimiwa wote, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuja kuniona hata wale washabiki wa Yanga pia walikuja kuniona. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia niishukuru familia yangu ikiongozwa na wake zangu kwa kunisimamia pamoja na kaka zangu. Lakini pia niwashukuru wananchi wa Jimbo la Mfenesini kwa kuja kuniangalia na sasa nipo salama. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, pia niwashukuru madaktari wakiongozwa na Dkt. Marijani na Dkt. Yussuf na wahudumu wote. Kwa kweli wana huduma nzuri sana pale Mnazi Mmoja. Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba nijibiwe swali langu Nam. 55.

**Nam. 55**

**Kutokamilika kwa Visima vya Ras-Al-Khaimah**

**Mhe. Machano Othman Said -** Aliuliza:-

Katika siku za hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipata msaada wa kuchimbiwa visima vya maji 150 kutoka Utawala wa Ras-Al-Khaimah. Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa mradi huo wa uchimbaji wa visima haukufikia malengo hali iliyosababisha wananchi wengi kuendelea kukabiliwa na shida ya maji katia maeneo mbali mbali.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea mradi huo kukwama.
(b) Ni visima vingapi vimechimbwa na kuanza kutumika kwa Unguja na vingapi kwa Pemba.
(c) Ni kiasi gani cha fedha kilitumika kwa mradi huu.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Lakini na mimi kabla ya kumjibu naomba nimuombee kwa Mwenyezi Mungu aimarishe afya yake ili tuweze kushirikiana kujenga nchi yetu.

Mradi wa Ras-Al-Khaimah ni mradi wa uchimbaji wa visima kupitia Mkandarasi wa Kampuni ya *Chimba Well Drilling and Construction Company Ltd* kutoka Dar es Salaam ambaye ndie aliyechaguliwa na Ras-Al-Khaimah kufanya kazi hiyo. Kazi za utekelezaji wa mradi huu zimekamilika kwa uchimbaji wa visima mia moja na hamsini (150) katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba kwa awamu tofauti, ununuzi wa pampu na ujenzi wa matangi sita (6) ya zege ya ujazo wa lita 120,000 kila moja juu ya mnara wa mita sita yamejengwa Unguja pekee.

Mhe. Spika, mradi huu haukukwama, bali kazi zilizotarajiwa kutekelezwa ambazo nimezieleza katika maelezo ya awali hapo zote zimekamilika, isipokuwa baada ya kukamilika kwa kazi hizo, kazi iliyoendelea ni uendelezaji wa visima hivyo kwa ulazaji wa mabomba. Shughuli nyengine ni uingizaji wa pampu, ujenzi wa vibanda, ujenzi wa vichwa na mifuniko ya visima *(wellhead)* na upelekaji wa umeme kila mwaka kadri uwezo wa fedha unavyoruhusu.

Visima vyote vilivyochimbwa ni 150, hadi Januari, 2021 jumla ya visima 66 tayari vimekamilika na vinatoa huduma kwa jamii. Napenda kutoa angalizo kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba kati ya visima hivyo vilivyoendelezwa baadhi yake vimesita kutokana na hitilafu za kiufundi. Aidha, Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* inavifanyia matengenezo ya kawaida visima hivyo.

Kiasi cha fedha kilichotumika kuchimba visima ni jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 1.5 kupitia Mfadhili (Mtawala wa Ras-Al-Khaimah) na kwa upande wa uendelezaji kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar uchambuzi wake unaonekana hapo chini.

| S/Nam. | Mwaka waFedha | Fedha iliyopangwa | Iliyopatikana/Iliyotumika | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2017/2018 | 1,500,000,000 | 1,500,000.000 | 100 |
| 2. | 2018/2019 | 4,000,000,000 | 2,464,206,000 | 62 |
| 3. | 2019/2020 | 3,000,000,000 | 2,016,589,570 | 67 |
| 4. | 2020/2021 | 4,000,000,000 | 551,103,514 | 14 |
| | **Jumla:** | **12,500,000,000** | **6,533,899,084** | **52** |

**Mhe. Machano Othman Said:** Ahsante Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini kabla ya kumuuliza swali la nyongeza naomba anifikishie salamu zangu kwa Katibu Mkuu kwa kazi yake nzuri aliyotufanyia Jimbo la Mfenesini, ni Katibu Mkuu ambaye ana mwelekeo na tuna matumaini sana na wizara yako.

Baada ya salamu hizo naomba kuuliza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa mradi huu ulikuwa unasimamiwa na Ras-Al-Khaimah na kwa vyovyote vile ulikuwa na muda maalum, na kwa sababu katika Jimbo la Mfenesini visima vitano vilivyochimbwa na Ras -Al- Khaimah, vinne vikitokea katika Shehia ya Chuini ambacho kimoja kimekwenda kuchimbwa kwenye ziwa na hakionekani na kisima kimoja kimechimbwa Mwakaje na Mwachealale nacho hakifanyi kazi, yaani visima vitano vyote havifanyi kazi. Na kwa kuwa Jimbo la Mfenesini lina visima 17 ambavyo vinafanya kazi ni vitatu tu pamoja na visima vyengine.

Kwa sababu Bumbwisudi tuna visima saba (7) vyote vinapeleka maji mjini, Selem kuna visima viwili (2) kimoja kibovu, tuna kisima Mfenesini Kivuma ndio kizima chenyewe, tuna kisima Melinane kibovu. Sasa kwa kuwa ukombozi wa wananchi wa Mfenesini ni visima vya Ras- Al-Khaimah tuna visima vitano (5) ambavyo vyote havifanyi kazi.

a) Je, Mhe. Waziri anatuahidi nini katika kuhakikisha kwamba visima vile vinafanya kazi ili wananchi wa Mfenesini waepukane na tatizo la maji.

b) Mradi huu ulianza zaidi ya miaka sita. Je, lengo lake ilikuwa utekelezwe kwa miaka mingapi na sasa imebakia miaka mingapi ili kukamilisha mradi huu.

c) Kwa kuwa wananchi wa Mfenesini wameathirika na ujenzi wa barabara kwa kuondolewa mabomba ya maji katika Shehia ya Mfenesini, Kama na Chuini pamoja na Kihinani. Ni lini serikali itarejesha miundombinu ile ya mabomba katika maeneo hayo.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Hili suala la pili kidogo naomba sikulipata.

**Mhe. Spika:** Jibu swali la (a) na (b), swali (c) liwache.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Kuna (a), (b) na (c) hilo (b) ndio sikulipata, naomba lile (b).

**Mhe. Spika:** Mhe. Machano uliza tena swali (b). Mhe. Machano swali (b) lilikuwa swali gani?

**Mhe. Machano Othman Said:** Niliuliza kwa sababu mradi wowote unakuwa na muda maalum na kama umechelewa unakuwa unaongezewa muda. Huu mradi wa Ras-Al-Khaimah ambao umeanza zaidi ya miaka sita iliyopita, ulikuwa wa muda gani na lini unatarajiwa kumalizika.

**Mhe. Spika:** Jibu mawili tu Mheshimiwa usijibu matatu.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nikiri kwamba katika Jimbo la Mfenesini vipo visima hivi kumi na saba (17) na visima vingi havifanyi kazi. Lakini nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba serikali kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* ina

mpango wa kuvifanyia matengenezo visima vyote hivi katika Jimbo la Mfenesini. Na kama alivyoniambia nilimtuma Katibu Mkuu kuanza kufuatilia jimboni ili kujua nini tufanye kuweza kuondoa kadhia hiyo katika jimbo hilo.

Suala la pili Mhe. Spika, mradi huu wa Ras-Al-Khaimah kama nilivyoeleza katika jibu mama ulishamaliza muda wake kwa yule mfadhili kazi yake ilikuwa ni kuchimba visima, alichimba visima 150 akanunua pamoja na pampu ambazo tulianza kuzitumia, lakini kwa bahati mbaya pampu zile hazikuwa na ubora nyingi ziliharibika mapema. Kwa hivyo, juhudi ya serikali ni kutafuta pampu za uhakika ili kuviendeleza visima hivi vya Ras-Al-Khaimah.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake lakini na hatua zake njema anazozichukua katika kuhakikisha wananchi wetu wanapata maji Zanzibar nzima ana jitihada kubwa sana.

Lakini pamoja na hivyo Mhe. Spika, katika Jimbo la Chumbuni tumepata faida ya visima hivi vya Ras-Al-Khaimah na vipo ambavyo vimeungwa na kuwapelekea wananchi maji. Lakini cha kusikitisha maji haya huwa yanatoka kuanzia saa nane au tisa usiku na kwa sisi tunaoishi Chumbuni muda huo tunakuwa tuna shughuli nyengine za visomo pamoja *kiamulail.*

Je, Mhe. Waziri, utafanya jitihada gani za dharura ili kuhakikisha maji tunayapata wakati wa mchana ili ule usiku tufanye zile shughuli ambazo zinaingia kwenye *kiamulail, zikri* na mambo mengine.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, naomba niendelee kukiri kwamba bado zipo dosari kwenye miundombinu ya maji lakini Serikali kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini inafanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba matatizo kama hayo tunayaondoa. Nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba nitakuwa pamoja nae kupita katika maeneo hayo ili tuone matatizo yaliyopo tuweze kuyasawazisha na yeye aendelee na *kiamulail* na shughuli nyengine za usiku.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa tunaomba utulivu kidogo.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa kweli amekuwa akitupa ushirikiano mkubwa sana na tulipompelekea kilio cha wananchi wa Jimbo la Mwanakwerekwe katika suala hili la maji, muda mfupi tu alituma maafisa wake wakaja jimboni wakafanya upembuzi yakinifu.

Lakini swali langu liko hapa. Je, ripoti ile ambayo tayari imeandaliwa utekelezaji wake utaanza lini.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Samahani Mheshimiwa ripoti gani?

**Mhe. Spika:** Ripoti mliyoitayarisha mnaanza kuitekeleza lini?

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Sijaijua ripoti gani.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Katibu Mkuu alituma timu ya maafisa wake jimboni kwa ajili ya kuangalia changamoto za maji kwenye maeneo tofauti na baadae maafisa walirejesha ile ripoti.

Je, ni lini ataweza kutukamilishia utekelezaji wake ule kwa ajili ya kutatua hizi changamoto. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, taarifa ya utekelezaji kutoka Jimbo la Mwanakwerekwe ipo kwa Katibu Mkuu kwa utekelezaji na tayari ameshatoa maelekezo kwa *ZAWA* kwa ajili ya kutekeleza maagizo yote ambayo yametokana na taarifa hiyo. Nikuahidi kwamba ndani ya muda mfupi ujao kabla ya bajeti tutakuwa tumefanya marekebisho katika eneo hilo.

**Nam. 85**

**Tatizo la Kukosa Maji Safi Shumba Mjini**

**Mhe. Shamata Shaame Khamis** - Aliuliza:-

Wananchi wa Shumba Mjini wanakabiliwa na changamoto ya kukosa huduma ya maji mara kwa mara, hii inatokana na bomba la maji lililokatisha chini ya bahari kuwa na viungo chini ya maji na kutokana na mkondo wa maji kusukuma na hatimae kukatika viungo hivyo.

a) Je, ni lini zitachukuliwa hatua kuondosha kadhia hiyo.

b) Je, ni kiasi gani cha fedha zinazohitajika kwa kazi ya kuondosha tatizo hilo.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 85 lenye kifungu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wananchi wa Shumba Mjini hawana kawaida ya kukosa maji mara kwa mara kama ilivyoelezwa. Katika hali ya kawaida kukatika kwa huduma ya maji husababishwa na mambo matatu makubwa ikiwemo, kuzimika kwa umeme, kupasuka kawaida kwa bomba au kwa kupasuliwa na wananchi wanaotumia eneo hilo kwa shughuli zao za uvuvi. Hali hii inaleta shida. Hata hivyo, *ZAWA* huwa inafanya marekebisho haraka iwezekanavyo inapotokea hali hiyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) *ZAWA* inatarajia kulitoa bomba hilo ambalo limeathiriwa sana na kuweka jengine jipya katika muda mfupi.

b) *ZAWA* itakuwa inalifanyia matengenezo bomba kadri hali inapojitokeza na wakati huo huo ikitafuta suluhisho la kudumu kwa kulibadilisha na kuweka

jipya ambalo litaweza kufanyiwa kazi ndani ya robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, kabla sijamuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza naomba nitoe maelezo mafupi. Nimuombe tu Mhe. Waziri huyo ambaye anamsaidia katika kutoa majibu ndani ya Wilaya ya Micheweni basi kidogo amfuatilie aweze kumjua kwa kina ana lengo gani kwa sababu mimi naishi huko na nimefuatilia kwa kina. Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo nina maswali nilitaka kujua tu.

(a) Je, Mhe. Waziri ni lini atakuja jimboni kwangu ili mimi na yeye tufuatane mguu kwa mguu twende tukaone hali halisi ya changamoto zinazowakabili wananchi wa jimbo hilo hususan hapo Shumba Mjini.

(b) Mhe. Spika, nilitaka kujua pamoja na matengenezo haya aliyosema kwamba yatafanyika. Nilitaka kujua ni kiasi gani cha fedha za serikali ambazo zinatarajiwa kutumika katika marekebisho hayo.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:**

(a) Mhe. Spika, nipo tayari kufuatana na Mwakilishi kuelekea Jimbo la Micheweni katika vitongoji vyote ikiwemo eneo la Shumba Mjini, linalokatisha bomba kutoka Kijichame kama itakuwa sijakosea kuelekea Shumba Mjini ambapo kuna bandari yetu ndogo pale. Nipo tayari kufanya ziara nae Mhe. Spika.

(b) Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba bomba hili tayari tumeshalinunua na kilichobaki ni kuliweka tu katika ile sehemu. Fedha zilizotumika naweza kukuletea kwa maandishi lakini tayari bomba limeshafika kisiwani Pemba wakati wowote litawekwa katika eneo hilo.

**Mhe. Mihayo Juma N'hunga:** Mhe. Spika, kwanza nianze kupongeza majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa jitihada zake binafsi za kuhakikisha anapambana kupeleka *resource* hii ya maji kwa wananchi nikiamini mpaka jana usiku tunazungumza nae yupo katika eneo la Machui kuhakikisha wananchi wa maeneo yetu wanapata maji.

Lakini pamoja na pongezi zangu hizo naomba kumuuliza swali langu moja dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa sababu bado kadhia ya maji imekuwa ni tatizo kubwa sana katika maeneo yetu hususan Jimbo langu la Mwera maeneo ya Kianga, Muembemchomeke, Shehia ya Mwera, Shehia ya Chemchem na Shehia ya Mtoni Kidatu bado kuna changamoto kubwa sana ya maji. Je, ni lini sasa Mhe. Waziri kupitia Mamlaka yako ya *ZAWA* itakuwa tayari kwenda kuweka miundo mbinu mipya ya maji hasa Shehia ya Mtoni Kidatu, Mtoni Chemchem na Kianga. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Ahsante Mhe. Spika, kwanza nikubaliane nae kuwa jana nilikuwa katika jimbo lake lakini sikuomba ruhusa, lakini nilikuwa katika harakati za kutafuta hiyo huduma ya maji.
Mhe. Spika, nikiri kwamba bado changamoto ya maji katika majimbo mengi ya Unguja na Pemba ipo lakini niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba kama alivyoanza kueleza

mimi mwenyewe napita maeneo yote kuhakikisha tunajua zile changamoto na namna ya kuzitatua.

Katika jimbo lake Jumamosi hii inayofuata *in shaa Allah* nimepanga kuanza kubadilisha baadhi ya miundombinu katika jimbo hilo ili kuweza kuhakikisha upatikanaji wa huduma hii ya maji kwa urahisi zaidi.

**Nam. 90**

**Ujenzi wa Barabara ya Buyu kwa Kiwango cha Lami**

**Mhe. Suleiman Haroub Suleiman** - Aliuliza:-

Katika kipindi cha Awamu ya Sita ya Uongozi wa Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume imetolewa ahadi ya ujenzi wa barabara ya Chukwani - Buyu kwa kiwango cha lami. Ahadi hiyo imetolewa na Rais Mstaafu huyo wakati akifungua Tawi la CCM Buyu mwaka 2010.

Je, serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa ahadi hiyo.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 90 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume alitoa ahadi ya ujenzi wa barabara ya Chukwani - Buyu kwa kiwango cha lami mwaka 2010. Hata hivyo, kutokana na Mpango Mkuu wa Viwanja vya Ndege *(Mas0ter Plan)* uliotayarishwa na wizara katika mwaka 2018/19 imeonekana kwamba barabara hiyo imo ndani ya eneo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Hivyo, serikali kwa sasa haina mpango wa kuijenga barabara hiyo na badala yake ina mpango wa kuijenga barabara ya Kisauni-Shakani-Buyu-Fumba ambayo tayari imeshafanyiwa Upembuzi Yakinifu. Barabara hiyo itakapojengwa itawasaidia wananchi wa maeneo hayo kupata huduma kwa urahisi na pia kama tunavyojua kwamba Fumba ni eneo la uwekezaji hivyo barabara hii itasaidia katika eneo la uwekezaji. Ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Suleiman Haroub Suleiman:** Mhe. Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Serikali ya Zanzibar ya Awamu ya Nane. Lakini pia ile kauli ya "Yajayo ni neema tupu" naiona hapa nimeridhika na majawabu yake. Naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo tu la nyongeza. Ni lini.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, kwa sasa serikali kupitia Wizara ya Nchi (OR) Fedha na Mipango tayari tumeomba fedha kupitia *ADB* pamoja *China Aid* kwa ajili ya kujenga barabara hiyo. Kwa hiyo, fedha zikiingia tu tutajenga barabara hiyo.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Ahsante Mhe. Spika na mimi kwa kuniruhusu kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa tayari wameshafanyia upembuzi yakinifu katika barabara hiyo ambayo inapitia Shakani-Buyu-Fumba na kwa vile wamefanyia huo upembuzi yakinifu moja katika upembuzi wao katika barabara hiyo inapopita kuna makaazi ya watu. Je, ni vipi wamewafanyia tathmini na itakuwaje katika malipo ya hao wananchi wanaoishi katika maeneo hayo ya Kisauni kupitia mpaka ikafika Fumba.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Mwanaasha Khamis Juma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, tutalipa fidia kwa mujibu wa utaratibu ambao upo katika wizara kwa vile tukijenga tunakuwa tunalipa fidia. Kwa hivyo, katika barabara hii pia tutafanya utaratibu wa malipo yote ambayo yapo katika fidia na wananchi watalipwa *in shaa Allah.*

**Mhe. Juma Ali Khatib:** Mhe. Spika, ahsante nampongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini tulikuwa tunakumbuka kwamba hiyo barabara aliyosema kwamba inapita *Airport* hii ilikuwa ni barabara katika iliyoombwa kwa mfuko wa *Emirates*.

(a) Je, Mhe. Waziri amekaa na wataalam wa wizara yake wakamhakikishia katika mpango huu wa serikali itapita Uwanja wa Ndege.

(b) Halafu hii barabara aliyosema ya Shakani pamoja na kwendea Buyu Mhe. Spika, kuna wananchi wanakaa Kisauni kutoka pale Mkunazi Samaki wakiunganisha hii barabara inayokwenda Shakani hawa ni wakulima wa mboga mboga. Hata Mwakilishi wa Jimbo la Kiembesamaki anafahamu kama kuna wakulima wengi kule wa mazao ya nyanya, tungule, mchicha. Je, Mhe. Waziri anaonaje sasa katika wizara yake kuunganisha barabara hii kutoka Mkunazi Samaki mpaka Shakani ili kuwarahisishia wale wakulima wetu kuweza kupata usafari kwenda sokoni kuuza mali zao. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Juma Ali Khatib swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza, nataka nimfahamishe tu mheshimiwa kwamba barabara ya Chukwani-Buyu imeondoshwa kwa sababu imeingia katika *master plan* kama nilivyosema mwanzo na tayari katika mpango mkuu baada ya miaka ishirini itajengwa *Airport* ndogo ya ndege ndogo ndogo. Kwa hivyo, iko upande wa mashariki ambayo iko hiyo barabara. Kwa hiyo, tayari hilo tumeliona na tumeona tukiitengeneza barabara ile itakuja kuleta matatizo baadae. Kwa hivyo, tumeona bora tuiwache tujenge sehemu nyengine.

Mhe. Spika, kwa upande wa swali (b) naomba kulichukua tutakwenda kulifanyia upembuzi zaidi.

**Nam. 30**

**Matengenezo ya Hospitali ya Wilaya ya Makunduchi**

**Mhe. Salma Mussa Bilal -** Aliuliza:-

Pamoja na Serikali kustahiki pongezi kwa kuzipandisha daraja Hospitali za Kivunge na Makunduchi kuwa Hospitali za Wilaya bado kuna changamoto katika hospitali hizo.

Ni lini Hospitali ya Makunduchi itafanyiwa matengenezo ili iweze kuendana na hadhi yake ya kuwa Hospitali ya Wilaya.

a) Je, ni lini Hospitali za Makunduchi na Kivunge zitajengewa ukuta ili kuziweka katika mazingira mazuri na kudhibiti uharibifu.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto) -** Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara inaendelea kuchukua juhudi mbali mbali za kuifanya Hospitali ya Makunduchi iendane na hadhi ya kutoa huduma za Hospitali za Wilaya, ambapo baadhi ya sehemu zilifanyiwa ukarabati ikiwemo wodi ya wanawake na chumba cha kusafisha mimba zilizoharibika, ambapo ukarabati huo umekamilika katika mwaka uliopita (2020).

Kwa muendelezo huo huo, Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022, imepanga kuendelea kufanya matengenezo, kujenga maabara pamoja na jengo jipya la huduma za dharura kwa lengo la kupunguza rufaa za ndani na pia kuwapatia huduma hizo wananchi karibu na maeneo yao. Aidha, suala la ujenzi wa uzio kwa Hospitali za Kivunge na Makunduchi tayari limo katika mpango wa Wizara na litatekelezwa pale tu fedha zitakapopatikana. Ahsante sana.

**Mhe. Salma Mussa Bilal:** Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe.Spika, kwa kuwa Wodi ya Wazazi ya Makunduchi iko chini ya njia kuu ambayo inapita magari na waendao kwa miguu, na kwa kusaidia juhudi za serikali na kuona umuhimu wa kujengwa uzio katika Hospitali ya Makunduchi, sisi Wawakilishi na Wabunge wa Viti Maalum tulichangia saruji mifuko mia. Mhe. Mwakilishi alichangia saruji mifuko thelathini na Mhe. Mbunge aliyepita alichangia mawe kwa ajili ya ujenzi wa uzio huu.

Swali langu ni hili hapa. Je, ni lini serikali itachukua hatua za dharura angalau kwa upande ule wa njia kuu kujenga uzio, ili kuweza kuwawekea stara akina mama ambao wanakwenda kujifungua katika hospitali ile.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto)**: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza nikiri kwamba tunazo changamoto za masuala ya uzio katika maeneo tofauti ya taasisi zetu za serikali na hili linatokana kwamba kiu ya kutoa huduma kwa wananchi na tunapoanza katika miradi hii tunakuwa tunaangalia ujenzi wa ndani kwanza halafu tunakuja kuangalia kote.

Sisi kwa upande wa serikali sasa hivi katika ujenzi tunaopanga katika mikakati yetu chochote ambacho tunachojenga tunahakikisha kwamba katika *plan* zetu basi na uzio inakuwemo. Mimi nimpongeze sana Mhe. Mwakilishi wa Viti Maalum pamoja na Mhe. Mwakilishi

mwenye dhamana katika jimbo kwa kuunga mkono juhudi za serikali, huu ndio ndio utaratibu na ustaarabu ambao sisi kwa upande wa serikali tunathamini mchango huu hasa wa wawakilishi wa wananchi.

Nimuombe Mhe. Mwakilishi awe mvumilivu suala hili tunalichukulia kwa uzito na pale endapo fedha tutakuwa tunazo kwa upande wa wizara, basi tutalifanyia kazi kwa haraka na nimuahidi hili jambo tutalichukua kwa uzito. Ahsante sana.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza serikali kwa kuona iko haja ya kuifanyia marekebisho makubwa Hospitali ya Chake Chake ili nayo iendane na hadhi ya Kiwilaya lakini tumeshuhudia ujenzi huo ukisuasua.

(a) Je, Mhe. Waziri unawaambia nini wananchi wa Chake Chake ili kupunguza masafa ya kwenda kutafuta matibabu Hospitali ya Mkoani au Abdalla Mzee.

(b) Je, ni lini ujenzi huu wa Hospitali ya Chake Chake utakamilika. Ahsante sana mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto)**: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shadya Mohamed Suleiman swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Swali lake la kwanza ni wananchi watarajie kitu gani.

Mhe. Spika, kwanza nimhakikishie kwamba katika kipindi hiki cha Mhe. Rais Dkt. Hussein Ali Mwinyi wananchi watarajie maneno yetu maarufu ambayo ni "Yajayo ni neema tupu". Kwa hiyo, hilo ndio jambo la kwanza la kuwaambia wananchi wake.

Lakini katika suala zima la kazi hii katika sekta ya afya katika miradi ambayo tuliyokuwa serikalini. Mhe. Spika, inawezekana katika awamu hizo saba kama nilivyojibu jana hapa kama wengine walinisikia kwamba sasa hivi tuna-*review* mikataba yetu mingi katika taasisi tofauti na miradi ambayo tuliyoingia. Lakini pia tunajaribu kuangalia katika kila jambo tunalolifanya kuweza kulipima. Ndio maana Mhe. Rais ametuagiza kwamba katika miradi yote katika kila Wizara na hakulisema hili kwa kujificha, amelisema hadharani kabisa mikataba yote na *project* zote ambazo zipo ndani ya serikali tuweze ku-*review* kutoka kubwa mpaka ndogo na kila fedha ambayo itakayotumika iende katika kuhakikisha inaleta tija.

Sasa mimi nimhakikishie tu kwamba kusuasua maana yake ni kwamba kila kitu kinataka kutengenezwa ili kiwe bora zaidi. Kwa hiyo, mimi nimuombe awe mvumilivu serikali ipo kazini, sisi tutahakikisha kwamba huduma zote hizi katika suala la afya na menginevo basi wananchi wanapata kama inavyostahiki, sio tu katika Hospitali ya Chake Chake, mradi wa Binguni, Wete na kwengineko kote. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake ya kuridhisha kwa kweli anakuwa na utulivu kiasi fulani.

Mhe. Spika, miongoni mwa ujenzi wa Hospitali yetu ya Chake Chake kunaonekana kusuasua sana. Lakini pili ujenzi ule kuna kitu wanaita *incinerator* imejengwa kwa ajili ya kuchomea taka taka za hospitali ni bora wakitumia mashimo ya kawaida tunakuwa hatuna adhabu ya ule moshi, lakini wakitumia ile *incinerator* inakuwa ni balaa katika mji wa Chake Chake. Je, Mhe. Waziri lile *incinerator* limejengwa kitaalam na kwa gharama gani. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto)**: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi wa wananchi kutoka jimbo muhimu kwa upande wa Pemba la Chake Chake Mhe. Shaib Hassan Kaduara swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwanza napokea pongezi zake za utulivu wa majibu ninayojibu, lakini pia kwa kupongeza kwamba tunatoa majibu yanayostahiki.

Mhe. Spika, suala la Hospitali ya Chake Chake hapa leo wameuliza watu wawili, mimi mara nyingi nachukulia kwamba swali linapoulizwa mara nyingi ina maana ni kuikumbusha serikali kuongeza juhudi na *speed* katika suala zima.

Mimi katika suala hili nimuahidi Mhe. Mwakilishi tu kwamba nalibeba na sisi kama serikali tuko hapa mawaziri tutazidi kulifuatilia kwa pamoja tuangalie labda kutoka maeneo gani tuzidi kuyafanyia kazi kwa undani zaidi. Kama nilivyosema mwanzo swali lake linafanana na la Mhe. Shadya Mohamed Suleiman kwamba suala hapa ni kuangalia je, miradi hii fedha zinazotumika zinaendana katika maeneo mengi sio katika Sekta ya Afya tu, Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Elimu na mengineyo.

Lakini kuhusu *incinerator* ni kiasi gani kimetumika mimi kwa sasa nitakuwa sina taarifa hizo kwa sababu sikujipanga kuja na taarifa hizo hapa kujua ni *amount* gani ilitumika. Lakini tunatambua kwamba hapa kuna *incinerator* ilijengwa na kama ina tatizo ambalo linatoa bughudha kwa wananchi hii itakuwa sio sahihi. Ni muhimu sisi kama serikali kutambua kero kama hizi zinapoletwa. Kwa hiyo, mimi nimuahidi Mhe. Mwakilishi watendaji wetu wapo juu wanalisikia suala hili tutalianzia kazi mara moja kuweza kujua nini kinachosababisha katika *incinerator* hii ambacho kinaleta usumbufu katika maeneo husika. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 58**

**Kukithiri kwa Matatizo ya Udhalilishaji katika Jamii**

**Mhe. Habib Ali Mohamed -** Aliuliza:-

Tafsiri na uzito juu ya suala la udhalilishaji limekuwa tatizo kubwa kwa jamii hivi sasa.

(a) Je, Serikali ina mpango wa kuleta mswada wa marekebisho ya sheria zote za udhalilishaji ambazo zina upungufu wa utekelezaji wa kisheria.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha uchunguzi wa makosa ya udhalilishaji unafikiwa katika kiwango kilicho bora.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Kituo cha Huduma za Sheria Chake Chake kinaendelea kutoa huduma kwa jamii.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru Mhe. Mjumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kuona ipo haja ya mabadiliko ya sheria hii ili kukabiliana na tatizo la vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

(a) Mhe. Spika, kwa kuwa Serikali imetoa agizo la kuzipitia sheria zote ambazo zinaonekana kuwa na vikwazo katika utekelezaji wake zirekebishwe, hivyo kufuatia agizo hilo Wizara itahakikisha kwamba sheria zote zenye vikwazo katika utekelezaji wake zinafanyiwa marekebisho.

(b) Mhe. Spika, kuhusu suala la uchunguzi, Serikali kupitia vyombo vyake vya uchunguzi, vikiwemo Jeshi la Polisi na Kituo cha Mkono kwa Mkono imejipanga kwa kuongeza vitendea kazi vya kufanyia uchunguzi wa kisayansi pamoja na kujenga uwezo wa watendaji, ili waweze kutoa huduma bora na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

(c) Mhe. Spika, Kituo cha Huduma za Sheria Chake Chake ni moja ya miongoni mwa vituo vinavyotoa huduma kwa watu wenye matatizo yanayohusiana na sheria na kusaidia katika utatuzi wa migogoro. Kwa sasa kituo hicho kinakabiliwa na mgogoro kati ya Mwenyekiti wa Bodi, Wajumbe na Wafanyakazi ambao tayari umefikishwa katika vyombo vya kisheria. Hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi waiachie Mahakama iendelee na kazi yake. Aidha, katika kipindi hiki cha utatuzi wa mgogoro huo Serikali inawaomba wananchi kuitumia Idara ya Msaada wa Kisheria, Wasaidizi wa Sheria katika Ngazi ya Shehia na Wilaya na kupitia Jumuiya zao ili kutatuliwa changamoto zinazowakabili. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Habib Ali Mohamed:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa kuwa serikali imeshatoa agizo kwamba sheria zote ambazo ni vikwazo katika utekelezaji wake zifanyiwe marekebisho na katika kipindi hichi kifupi cha ndani ya mwezi mmoja nimesikia kesi mbili za udhalilishaji. Moja ikiwemo katika Jimbo langu la Mtambwe ambayo mtuhumiwa ameshafikishwa katika vyombo vya sheria na moja wiki iliyopita niliisikia hapa Unguja ambayo imo ndani ya familia yangu na mtuhumiwa vile vile ameshafikishwa katika vyombo vya sheria. Je, Mhe. Waziri kwa kuwa vitendo hivi vinauma, vinakera, vinaudhi, ni lini serikali itaileta sheria hii katika Baraza lako Tukufu ili kufanyiwa marekebisho. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Habib Ali Mohamed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi ya kumpa pole juu ya kesi ambayo imemkuta ndani ya familia. Kwa kweli Mhe. Spika, suala hili linauma na kama alivyosema yeye mimi nafahamu pia waheshimiwa wengi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wengine hata mambo haya yakizungumzwa yanakuwa yanawakera hasa wakina mama ambao wao linawaumiza sana suala hili. Hatusemi kwamba kina baba haliwaumi lakini kuna uchungu wa hali ya juu. Hata sisi kwa upande wa serikali kuyajibu maswali kama haya yana kero yake pamoja na hata viongozi ambao yanawakuta haya.

Mhe. Spika, suala la udhalilishaji ni suala ambalo kero kwa kweli na kama nilivyosema kwa sababu suala hili lilikuwa na masuala mengi katika Baraza hili katika maeneo tofauti. Na nikajibu juzi pia sheria ambazo zinasimamiwa katika utaratibu mzima wa suala zima la udhalishaji ambazo nilisema kuhusu suala la *Universal Declaration of Human Rights* ambao ni haki za watoto na kimoja ni Sheria ya Mtoto ya Nam. 6 ya 2011, Sheria Nam. 7 ya 2018 na Sheria ya Ushahidi ya mwaka 2016 ambayo sasa pia kuna sheria ndogo ndogo jana tumezifanyia marekebisho kuweza kwisha kwa masuala mengine ambayo yatakuwa watu wanakosa dhamana.

Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba katika suala zima la udhalilishaji nilijibu juzi katika suala la elimu, pia kwa upande wa afya ni suala mtambuka, vita hivi ni vikubwa sana kwa sababu mdudu huyu na shetani huyu aliyeingia katika jamii hadi hivi sasa tunapambana nae unakuta ni mbaya. Kwa hiyo, sisi kwa upande wa serikali inabidi tunaendeshwa kwa mujibu wa katiba na sheria, tutaendelea kutoa elimu kupambana kuungana nguvu kwa ujumla na tusichoke na tusirudi nyuma kamba na nguvu tuliyoanza nayo twende nayo hii hii mpaka tuweze kumtokomeza katika jamii pia. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, imeonekana kwamba hizi kesi zilikuwa ni nyingi sana hasa kwa huko tulikotokea, lakini sasa hivi tuseme "Yaliyopita si ndwele tugange yajayo".

Je, Mhe. Waziri ni idadi ya kesi ngapi na matukio mangapi yaliyoripotiwa tokea Mhe. Rais mpya wa awamu hii alipokaa madarakani na kuonesha ari yake ya kuchukizwa sana na vitendo hivi vya udhalilishaji.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Zawadi Amour Nassor swali lake la nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Zawadi Amour Nassor maswali yake yanakuwa mafupi lakini magumu, nikisema magumu kwamba yanahitaji kuwa na taarifa zaidi. Lakini niseme tu kwamba katika mwezi wa Januari juzi tulitoa taarifa zetu kwa upande wa mambo ya udhalilishaji katika maeneo tofauti zilikuwa mia na ishirini. Sasa yeye anataka takwimu tangu siku Mhe. Rais alipoapishwa ina maana hapa ni kutoka awamu ya saba kwenda awamu ya nane bila ya kukosea saa na muda wenyewe. Kwa hiyo, ili kutaka kumrahisishia nitampatia takwimu hizi kwa maandishi katika maeneo tofauti ya kiwilaya na mkoa kwa visiwa vyote vya Unguja na Pemba. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 70**

**Matumizi ya Kielektroniki katika Sekta ya Afya**

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum -** Aliuliza:-

Mradi wa *E-Government* pamoja na malengo mengine, ulikusudia kuhakikisha kwa matumizi ya njia za kielektroniki katika Sekta ya Afya.

Je, ni maeneo gani mpaka sasa yamefanikiwa katika mradi huo kupitia Sekta ya Afya.

**Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto (Kaimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 70 kama ifuatavyo:-
Mhe. Spika, mradi wa *E-Health* ni moja ya miradi iliyomo katika miradi mikubwa ya *E-Government*, ambayo pia unahusisha mradi wa *E-Tax*.

Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Kampuni ya *ZTE* kutoka China.

Mhe. Spika, katika kutekeleza mradi wa *E-Health*, vituo 18 (95%) kati ya vituo 19 (kutoka Wilaya 10 Unguja na Pemba) vilivyopangwa vimeunganishwa kwenye mkonga wa serikali. Kuunganishwa kwa vituo hivyo na mkonga kunarahisisha upatikanji wa mawasiliano ya moja kwa moja kwa vituo vilivyounganishwa kuweza kutumia mifumo yote ya kiafya bila ya kutumia *internet*.

Mhe. Spika, kupitia mradi huu mifumo mbali mbali ya kielektroniki ya afya imetengenezwa ikiwemo mfumo wa *PACS*, ambao unawezesha wataalamu wa Mionzi (*Radiologist*) wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuzisaidia Hospitali za Vijiji, Wilaya na Mkoa kufanya huduma za uchunguzi *(Diagnosis)* kupitia mtandao na kutuma majibu kwenye hospitali husika. Mfumo mwengine ni wa *Telemedicine* huu pia unawasaidia watoa huduma za afya kupata ushauri na msaada wa kitaalamu kutoka kwa madaktari bingwa ndani na nje ya nchi kupitia mtandaoni pale inapohitajika. Aidha, sambamba na mifumo hiyo wizara pia imeweza kutengeneza mfumo wa *EMR* unaotumika katika kukusanyia taarifa za wagonjwa.

Mhe. Spika, kwa upande wa ununuzi wa vifaa vya matibabu wizara imefanikiwa kufunga vifaa tiba vya kileo katika hospitali mbali mbali Unguja na Pemba. Vifaa hivyo ni pamoja na *MRI* (1) iliyofungwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ("*Digital Radiology System*" (4) zilizofungwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja (2), Kivunge (1) na Makunduchi (1), *mobile machine* za *X-Ray* (3) zilizowekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja (2) na Abdalla Mzee (1), viti vya kung'olea meno (5) vyenye mashine ya *X-Ray* vilivyofungwa katika Hospitali ya Makunduchi (2), Wete (1), Micheweni (1) na Kituo cha Fuoni (1), *Table Ultrasound Machine* (3) zilizofungwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja (2) na Kivunge (1), *Portable Ultrasound Machine* (4) zimewekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja (2), Kivunge (1) na Chake Chake (1).

Mhe. Spika, vifaa vyengine ni *Anaesthesia Machine* (15) zilizowekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja (10), Kivunge (1), Makunduchi (1), Micheweni (1), Wete (1) na Chake Chake (1), *Patient Monitor* (8) zilizowekwa katika Hospitali ya Kivunge (2), Makuduchi (2), Chake Chake (2) na Micheweni (2), *Oxygen Concentrators* (14) zilizowekwa katika Hospitali ya Micheweni (2), Chake Chake (2), Abdalla Mzee (4), Makunduchi (2), Kivunge (2) na Mnazi Mmoja (2), jokofu za kuwekea damu (5) zilizowekwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja (2),

Makunduchi (1), Abdalla Mzee (1) na Micheweni (1) na vingi vyenginevyo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Spika na namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake, mbali ya majibu hayo nina hakika Mhe. Waziri atakuwa bado hata na yeye sijui kama atakuwa anaelewa hii mifumo ya *PACS* na *EMR* iko *too medical*, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mhe. Spika, lengo la *E-Health* ni zuri sana na tunapata faraja kuona kwamba sasa hivi hii *system* inafanya angalau katika *primary stage* kwa *information* ya magonjwa na wagonjwa wenyewe imekuwa inafanya kazi vizuri. Mhe. Spika, swali langu ni kwamba *currently* tukienda kwa mfano Dar es Salaam katika kitengo cha *cancer* utakuta bado kuna akina mama ambao wanatoka Zanzibar na watoto wapo kule, lakini ingewezekana kama *E-Health* ikawa inafanya kazi vizuri kwamba matibabu ya kansa na magonjwa mengine hususan kwa watoto ikawa yanafanyika hapa Zanzibar kwa sababu wanapokwenda Dar es Salaam inakuwa ni gharama zaidi inabidi wazazi ndio wazibebe gharama hizo.

a) Mhe. Spika, kwa mpango huu lini wizara ama serikali itaanza kuona kwamba *telemedicine* inafanyika angalau tu kwa kuunganisha Hospitali ya Muhimbili na *Ocean Road* pamoja na Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kuanza kufanya matibabu ya wagonjwa wakiwa hapa hapa nyumbani.

b) Vifaa vimewekwa vingi sana na tunaipongeza sana serikali kwa hatua hii, lakini vile vifaa mimi juzi nilikuwa hospitali usiku, vifaa vipo lakini mazingira ya vifaa hayapendezi na hayako katika hali nzuri. Kwa maana hakuna *AC*, sehemu haziko nadhifu sana kwa ajili ya vile vifaa. Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba vifaa hivi viko katika mazingira mazuri ili viweze kutumika kwa muda mrefu zaidi kwa sababu *investment* iliyofanyika kwenye *E-government* ni kubwa sana mheshimiwa na ina-*incur* fedha za walipa kodi na wananchi wa Zanzibar. Lini tuna mpango wa kuweza kutengeneza mazingira mazuri ili vifaa viweze kutumika kwa muda mrefu zaidi. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto (Kaimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Dkt. Saada Mkuya Salum swali lake la nyongeza. Kwanza nitoe maelezo kadhaa kwamba nimueleze kuwa inawezekana mtu asiwe mtaalamu wa afya lakini katika Baraza hili kila mmoja ameingia kwa njia yake yeye ni mteule wa Mhe. Rais, humu ndani kuna watu ni wavuvi kuna wengine wa kilimo lakini ni wawakilishi wa wananchi wana ufahamu mkubwa. Kwa hiyo, anaposema kwamba inawezekana nisijue jambo sio kama sifahamu, kufahamu jambo jengine la pili ni kuelewa jambo...

**TAARIFA**

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Naomba niweke vizuri nilichokukisudia kusema kwamba hili jibu liko *too medical* kwa maana kwamba zile *terminology* sio kila mtu hata mimi mwenyewe sielewi *thus what I ask*, hakuna kitu kingine kilichotokezea.

**Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto (Kaimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):** Ahsante sana Mhe. Spika, sasa naomba nimjibu swali lake la

nyongeza. Mhe. Spika, swali la kwanza la *cancer* inawezekana Mhe. Mwakilishi hakufuatilia katika vyombo vya habari. Ni kwamba hapa Zanzibar mwaka huu ndio walikuwa wenyeji wa mkutano wa Jumuiya ya Madaktari Bingwa wa Saratani ambao ulifanyika katika hoteli ya Verde. Nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wake na watu wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia na Watoto tushiriki kwa pamoja sote. Pia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alitupa agizo moja kwa moja kwamba madaktari bingwa na yule Mwenyekiti wa Jumuiya yao tuanze kushirikiana kutoka pale tulipo sasa hivi katika awamu ya nane tuweze kwenda kwa pamoja.

Mhe. Spika, wametuahidi wale pamoja na madaktari wetu wote kukawa kuna ushirikiano wa hali ya juu, inawezekana tukija kufika kwenye suala la *telemedicine*, lakini sasa hivi katika suala zima la kutoa *experience* ya kwa daktari ambalo tayari linafanyika lakini lifanyike kwa ukubwa zaidi, mbali ya kupeleka madaktari wetu kwenda *Ocean Road* kwenda kufanya masuala ya training pia kuhakikisha kwamba sisi kwa upande wa Zanzibar vyuo vyetu tunashirikiana kwa pamoja. Kwa hiyo, hilo tayari linafanyika Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuhusu vifaa vya Mnazi Mmoja na vitendea kazi, mheshimiwa lazima tukiri na Mhe. Makamu wa Pili pamoja na Mhe. Rais wamezungumza katika maeneo tofauti kwamba suala zima la vifaa vyetu kwa sababu suala la utunzaji limekuwa tatizo katika taasisi nyingi za serikali, sio katika sekta ya afya au Mnazi Mmoja.

Mhe. Spika, mbali ya kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja imezidiwa kutokana na wingi wa watu kuwa rufaa na ndio maana Serikali hii ya Awamu ya Nane inazingatia sasa hivi kwa haraka kujenga hospitali mpya Binguni ili katika maeneo haya vifaa vitakavyowekwa viwe vinakwenda. Haiwezekani kila siku tunachukua eneo hilo hilo tunajenga sehemu tunaongeza, mimi Mhe. Spika nimefanya ziara Mnazi Mmoja kama nikiwa Kaimu Waziri naamini Waheshimiwa Wawakilishi wengi wamekwenda hata ukiingia katika Maabara yetu kule juu mashine ziwekwa nyingi sana kumezidiwa na lazima tukiri ndio maana Serikali ya Awamu ya Nane inataka kuamua katika sekta ya afya tuwe na hospitali kubwa zaidi ambapo pia na huduma katika maeneo mengine tuweze kuboresha.

Kwa hiyo, sisi tusimame hapa kama Waheshimiwa Wawakilishi tuendelee kulisemea suala zima la utunzaji. Lakini kwa upande wa serikali kujipanga upya katika suala zima la vifaa vyote, sio katika sekta ya afya tu ni maeneo yote. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante waheshimiwa maswali yamemalizika nina tangazo moja, Waheshimiwa Wajumbe naomba kukujuilisheni kuwa mara baada ya kugharisha kwa shughuli za Mkutano wa Baraza Wajumbe wa Kamati zifuatazo wanatakiwa wakutane kwa ajili ya kukamilisha zoezi la uchaguzi wa viongozi wa kamati, kamati zenyewe ni kama zifuatazo:

1. Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati hawa wakutane ukumbi Nam. 2 wa kamati;
2. Kamati ya Uchumi wakutane ukumbi Nam. 3 wa kamati;
3. Kamati ya Ustawi wa Jamii wakutane chumba cha *internet;*
4. Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika na Serikali za Mitaa wakutane kumbi mkubwa wa mikutano juu;
5. Kamati ya Bajeti wakutane *reading room*. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe.

## TAARIFA YA SERIKALI

**Hotuba ya Uwasilishaji wa Mgawanyo wa Rasilimali Fedha kwa Kipindi cha Januari - Juni kwa Mwaka 2020/2021 Kufuatia Mabadiliko ya Muundo wa Serikali**

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya Mgawanyo wa Rasilimali Fedha kufuatia mabadiliko ya muundo wa serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mhe. Spika, kufuatia kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa Serikali kumejitokeza mabadiliko ya muundo wa serikali ikiwemo mabadiliko ya wizara, idara na taasisi za serikali. Kwa kuwa mabadiliko haya yamejitokeza kati kati ya utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imelazimika kuandaa taarifa hii na kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu kwa mazingatio.

Mhe. Spika, taarifa hii inawasilisha mabadiliko ya mgawanyo wa rasilimali fedha kufuatia kutangazwa kwa wizara mpya ambazo zimesababisha baadhi ya idara kuhamia wizara nyengine na kuundwa kwa wizara mpya ambazo hazikuwepo hapo kabla. Kuhama kwa taasisi hizi kumepelekea serikali kufanya uhaulishaji wa bajeti kutoka wizara moja kwenda nyengine pamoja na kuchangia bajeti kwa wizara mpya katika kipindi cha miezi sita yaani cha kuanzia Januari hadi Juni 2021.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 42, fasili ya 1 na 2 vimempa mamlaka Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuunda serikali na kutangaza mawaziri mara tu baada ya kuapishwa. Kufuatia mamlaka hayo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo tarehe 19 Novemba, 2020 alitangaza wizara na Baraza la Mawaziri na kuitaka serikali kuanza kazi mara moja.

Mhe. Spika, kufuatia mabadiliko hayo yaliyojitokeza katika mafungu ya wizara na taasisi mbali mbali, Sheria ya Fedha na Umma Nam. 12 ya 2016, kifungu cha 51, fasili ya 1 na 3 vinamtaka waziri anayeshughulika na masuala ya fedha kuwasilisha taarifa juu ya mabadiliko hayo katika Baraza lako la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mabadiliko ya wizara ambayo yalihusisha idara na taasisi zake yamepelekea kufanya mabadiliko katika matumizi ya bajeti ya 2020/2021 iliyoidhinishwa na Baraza lako tukufu. Kwa hiyo, imelazimika kufanya marekebisho kwa kufanya uhaulishaji wa bajeti kwa wizara zilizoathirika. Uhaulishaji huo umezingatia bakaa ya bajeti za idara zilizohamishwa kutoka wizara moja kwenda wizara nyengine katika kipindi cha miezi sita cha kuanzia Januari hadi Juni 2021. Hivyo, mabadiliko ya mgawanyo huo ya rasilimali fedha haukuathiri bajeti kuu ya serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo iliidhinishwa na Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia mabadiliko hayo yaliyopelekea kuathiri kwa majina na makadirio ya bajeti za wizara zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2020/2021 Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango inawasilisha orodha ya muundo na bajeti ya wizara na taasisi kabla na baada ya mabadiliko kama ambavyo zinaonekana katika kiambatanisho Nam. 1 na Nam. 2.

Mhe. Spika, nawaomba wajumbe waipokee taarifa ya mabadiliko ya rasilimali fedha kufuatia muundo mpya wa serikali. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Anna Athanas Paul (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti):** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mbele yako hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na taarifa ya mgawanyiko wa rasilimali fedha kwa kipindi cha Januari - Juni katika mwaka wa fedha 2020/2021 kufuatia mabadiliko ya muundo wa serikali.

Mhe. Spika, kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutujaalia afya na uzima tukaweza kuendelea na majukumu yetu katika Baraza lako tukufu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (SW) atujaalie wepesi wa kutekeleza majukumu yetu pamoja na kuwaombea afya na uzima wale wote wanaosumbuliwa na maradhi mbali mbali na kuwaombea kheri waliotangulia mbele ya haki.

Mhe. Spika, napenda kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili ya kutoa maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusiana na taarifa ya mgawanyiko wa rasilimali fedha kwa kipindi cha Januari – Juni, 2020/2021. Ifahamike kwamba, taarifa hii imetokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1984 kupitia Kifungu cha 42(1) cha Katiba ya Zanzibar kinachompa uwezo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzisha wizara na kuunda serikali.

Mhe. Spika, baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitangaza wizara Mpya ikiwemo Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na baadhi ya idara kuhamishiwa katika wizara nyengine ili ziende sambamba na majukumu yaliyomo katika wizara hizo.

Mhe. Spika, mabadiliko haya yamepelekea serikali kufanya uhaulishaji wa bajeti kutoka wizara moja kwenda nyengine, pamoja na kuzichangia bajeti wizara mpya katika kipindi cha Januari – Juni 2020/2021.

Mhe. Spika, kifungu cha 107(2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinaruhusu matumizi kufanyika iwapo kutakuwa na maelezo ya ziada. Aidha, kifungu cha 51(1) na 51(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya 2016, vinampa uwezo waziri anayehusika na masuala ya fedha kuwasilisha mapitio ya bajeti kwa kipindi cha miezi sita katika Baraza la Wawakilishi iwapo kutafanyika marekebisho ya fedha baina na ndani ya mafungu au kuhamisha kazi kutoka taasisi ya umma moja kwenda kwa taasisi ya umma nyengine. Kwa msingi huo, Kamati ya Bajeti iliwasilisha maelezo ya ziada kuhusiana na matumizi yaliyotumika na yanayoendelea kutumika kwa kipindi cha Januari – Juni 2020/2021.

Mhe. Spika, naomba kulijuulisha Baraza lako tukufu kuwa mabadiliko ya mgawanyo wa rasilimali fedha yaliyofanywa na kuwasilishwa mbele ya Kamati ya Bajeti yamezingatia matakwa ya kikatiba na kisheria.

Mhe. Spika, Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kukutana na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kujadili taarifa iliyotoa ufafanuzi kuhusiana na Mgawanyo wa Rasilimali Fedha kwa Mapato na Matumizi ya Wizara na Taasisi kabla ya Mabadiliko ya muundo wa wizara na baada ya mabadiliko. Kiujumla mabadiliko hayo hayakuathiri Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2020/2021. Kamati inaipongeza Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kutupatia maelezo ya ziada kuhusiana na mabadiliko yaliyofanyika.

Mhe. Spika, kamati inaishauri wizara kuhakikisha mgawanyo wa mapato na matumizi unaendana na uhalisia wa wizara, idara na taasisi husika ili kuepusha kudhoofisha shughuli za idara na taasisi ambazo zina majukumu na mchango mkubwa kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, taarifa inayohusiana na Mgawanyo wa Rasilimali Fedha iliyowasilishwa katika kamati inaonesha namna ya matumizi ya serikali yanavyofanyika kwa kufuata misingi ya kikatiba na kisheria. Kamati inaunga mkono jitihada za serikali na inaziomba wizara, idara na taasisi zote zilizohusika katika mgawanyo huu, kufanya usimamizi madhubuti ili kuleta uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi yanayofanyika yaendane na malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine kamati inashauri fedha zinazopelekwa katika idara mpya zilizoanzishwa zitoke katika matumizi mengineyo na sio katika fedha za miradi ya maendeleo. Kwani kutumia fedha za miradi kunaweza kuchelewesha kumalizika kwa miradi hiyo.

Mhe. Spika, kamati inashauri kuwepo kwa fungu maalum kwa ajili ya kufidia mabadiliko yoyote ya kimuundo wa wizara ama idara, kwani kuchukua fedha kutoka katika idara iliyopo na kupeleka katika idara nyengine mpya kunaweza kuharibu mipango ya kibajeti iliyopitishwa awali na kukosa kufikia malengo.

Mhe. Spika, **k**amati inaweka msisitizo kwa Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuweka uchanganuzi wa fedha za wizara na idara mpya zinazopelekwa na sio mafungu ya jumla tu, ili kuziwezesha kamati kufuatilia utekelezaji wa bajeti pale inapohitajika kufanya hivyo.

Mhe. Spika, naomba nihitimishe kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa kupitia kwa umakini taarifa hii na kutoa maoni na ushauri kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa bajeti ya serikali. Aidha, napenda niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Bajeti kwa kutekeleza vyema majukumu yao ya kuratibu shughuli zote za kamati na na kuishauri kamati.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu niwatambue kwa majina Wajumbe na Makatibu wa Kamati kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Said Saleh Salim | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Anna Athanas Paul | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi Gavu | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Suleiman Haroub Suleiman | Mjumbe |
| 6. | Mhe Mwanaidi Kassim Mussa | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Harusi Said Suleiman | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Abdalla Ali Shauri | Katibu |
| 9. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 10. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |
| 11. | Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa naomba nichukue fursa hii tena kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati kuhusiana na Taarifa ya Mgawanyo wa Rasilimali Fedha kwa kipindi cha Januari – Juni 2020/2021 kufuatia mabadiliko ya muundo wa serikali. Aidha, napenda kuwashukuru wajumbe kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu wa hali ya juu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Anna Athanas Paul kwa uwasilishaji. Naomba sasa nimkaribishe tena mtoa hoja Mhe. Waziri kwa sababu sioni kama kuna mtu yeyote anayetaka kuchangia ili aje ahitimishe hoja yake. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, nashukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii, kwanza niishukuru na niipongeze kwa dhati kabisa Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Dkt. Saada Mkuya Salum kwa mashirikiano ambayo wanaendelea kutupa katika kufanikisha kazi zetu mbali mbali. Aidha, baada ya kusema hayo Mheshimiwa naomba kwanza niyapokee maoni yote ya kamati na kupitia Baraza lako tukufu nieleze haya yafuatayo:-

Kwanza, mgawanyo wa pesa tuliofanya kupeleka kwenye mafungu mapya tulizingatia mipango yote mikuu ya kitaifa ambayo inatuelekeza ikiwemo *Vision 2020* ambayo tunaimalizia, MKUZA III, pia ahadi mbali mbali za viongozi wetu wakuu na mpango wetu wa mendeleo wa mwaka 2020/2021. Kikubwa kama ambavyo Mhe. Anna Athanas ameeleza kwamba, kuna baadhi ya taasisi zilikuwa sehemu nyengine. Mathalan, kabla ya mabadiliko haya yaliyofanyika mwezi Novemba kulikuwa hakuna Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini taasisi zinazoiunda ile wizara zilikuwa maeneo mengine. Kwa hivyo, tulichokifanya sio kwamba tumetengeneza kitu kipya ni zile taasisi ambazo zilikuwa maeneo mengine zimekwenda kuunda wizara mpya.

Kwa mfano, kulikuwa na Idara ya Mazingira ambayo ilikuwa chini ya Afisi ya Makamu wa Pili ambayo inakwenda Makamu wa Kwanza, Wizara ya Fedha tulikuwa tuna kitengo cha *PPP* ambacho kilikuwa kina bajeti yake, lakini katika muundo huu mpya ukikiona kiko chini ya Wizara ya Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Kwa hivyo, hakuna kipya ndio maana tukasema hatujaathiri bajeti kuu. Kwa hivyo, malengo yote na *structure* yote ya kibajeti haikuathirika.

Mhe. Spika, pia kwa kusema hivyo ni kwamba, mafungu yote yale yana uchambuzi wake wa kina, kwa sababu hatukuhamisha *vote*, hizi *vote* zimeundwa na idara ambazo hapo kabla zilikuwa na mchanganuo wake wa pesa ambazo zilitengewa.

Pili, kama nilivyosema kwamba kutokana na hivyo hakuna pesa zilizohama kutoka kwenye miradi ya maendeleo kwenda kutumika kama pesa kwa ajili ya *recurrent budget*.

Baada ya kusema hayo, sasa Mhe. Spika, naomba sasa Baraza lako tukufu kupokea taarifa hii ya mgawanyo wa rasilimali fedha kufuatia mabadiliko ya muundo wa serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ambavyo inaelekezwa na Kifungu cha 51 fasili ya (1) na (3) ya Sheria za Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niwahoji wale wote wanaopokea hii taarifa wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Uchaguzi wa Viongozi wa Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola**

**Kanda ya Zanzibar (*CPA*)**

**Mhe. Spika:** Katibu nafikiri sasa tupe maelezo.

**Katibu:** Mhe. Spika, utaratibu wa uchaguzi wetu wa leo utakuwa tofauti kidogo na uchaguzi ambao ulifanyika kwa nafasi ya Wenyeviti wa Baraza, Naibu Spika na Spika, kwa maana ya kwamba katika chaguzi hizo nilizozitaja zina maelekezo ya kikatiba, kwa maana ya kwamba uchaguzi wake lazima uwe ni uchaguzi wa siri. Lakini kwa chaguzi zetu hizi za leo hakuna masharti ya kikatiba wala kisheria ambayo yanaelekeza chaguzi hizo kufanywa kwa njia ya siri. Kwa hivyo, Mhe. Spika tunapendekeza chaguzi hizi za leo zifanyike kwa njia ya *acclamation* kwa maana ya kwamba kuwahoji wajumbe kwa kila nafasi ili kuokoa muda.

Mhe. Spika, tutaanza na chaguzi ya *CPA* kwa maana ya Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya za Madola na tutaanza na nafasi ya mwenyekiti wa chama hicho. Nafasi hiyo Mheshimiwa imegombewa na mtu mmoja pekee ambaye ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kwa maana hiyo naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf wanyanyue mikono, ambao wanamkataa, Mhe. Nadir Abdul-latif ameshinda kwa kura zote. Tuendelee katibu. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika nafasi inayofuata ni nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (*CPA*) na mgombea wa nafasi hiyo ni mmoja pekee ambaye ni Mhe. Omar Said Shaaban.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wote wanaounga mkono nafasi hiyo kwa Mhe. Omar Said Shaaban wanyanyue mikono, wanaomkataa, Mhe. Omar Said Shaaban ameshinda kwa kura zote. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika, nafasi zinazofuata ni nafasi za wajumbe watatu wa Kamati Tendaji ya *CPA* na kwa bahati pia wajumbe watatu pekee ndio wamejitokeza kugombea nafasi hizo, ambao ni Mhe. Shaib Hassan Kaduara, Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Yahya Rashid Abdulla. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nitapiga kura zao wote kwa pamoja wanaowakubali wajumbe hao watatu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. Kwa hivyo, waheshimiwa wote hao wamechaguliwa. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika, kwa Chama hicho hicho cha *CPA* nafasi ya mwisho ni nafasi ya Mweka Hazina wa chama hicho nayo pia imegombewa na mjumbe mmoja pekee ambaye ni Mhe. Anna Athanas Paul. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa niwahoji wale wote wanaomuunga mkono Mhe. Anna Athanas Paul wanyanyue mikono, wanaomkataa, hakuna aliyemkataa na Mheshimiwa ameshinda kwa kura zote. *(Makofi)*

**Uchaguzi wa Chama cha Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumuiya ya Madola**

**Kanda ya Zanzibar (*CWP*)**

**Mhe. Spika:** Katibu tunaomba maelezo.

**Katibu:** Mhe. Spika, kwa Chama hicho cha *CWP* tunaanza na nafasi ya Mwenyekiti wa Chama hicho na aliyejitokeza kugombea ni mjumbe mmoja pekee ambaye ni Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante, wale wote wanaomuunga mkono Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum wanyanyue mikono, wanaomkataa. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum ameshinda kwa kura zote. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika, nafasi inayofuata ni nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa *CWP* ambayo nayo imegombewa na mjumbe mmoja pekee, ambaye ni Mhe. Anna Athanas Paul.

**Mhe. Spika:** Wale wote wanaounga mkono nafasi ya Makamu Mwenyekiti *CWP* Mhe. Anna Athanas Paul wanyanyue mikono, wanaomkataa, hakuna aliyemkataa kwa hivyo, mheshimiwa ameshinda kwa kura zote. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika, nafasi inayofuata ni ya Mweka Hazina wa *CWP* ambayo pia imegombewa na mjumbe mmoja pekee Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir. *(Makofi)*

**Mhe.Spika:** Wale wote wanaounga mkono nafasi ya Mweka Hazina Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir wanyanyue mikono, wanaomkataa, hakuna aliyemkataa kwa hivyo, mheshimiwa ameshinda kwa kura zote. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika, nafasi inayofuata ni Wajumbe watatu wa Kamati Tendaji ya *CWP*, nayo imegombewa na wajumbe watatu pekee Mhe. Harusi Said Suleiman, Mhe. Aza Januar Joseph na Mhe. Salma Mussa Bilal. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Naomba nihoji kwa wagombea wote kwa pamoja wanaowaunga mkono wanyanyue mikono, wanaowakataa, waheshimiwa wote watatu wamekuwa Wajumbe wa Kamati Tendaji. *(Makofi)*

**Uchaguzi wa Viongozi wa Umoja wa Wawakilishi wa**

**Kupambana na UKIMWI Zanzibar (UWAKUZA)**

**Mhe. Spika:** Katibu tunaomba maelezo.

**Katibu:** Mhe. Spika, katika Jumuiya ya UWAKUZA tunaanza na nafasi ya Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo nayo imegombewa na mjumbe mmoja pekee, Mhe. Shamata Shaame Khamis.

**Mhe. Spika:** Naomba niwahoji wale wote wanaomuunga mkono Mhe. Shamata Shaame Khamis kuwa mwenyekiti, wanaomkataa, Mhe. Shamata Shaame amekuwa mwenyekiti kwa kushinda kura zote. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika, nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa UWAKUZA imegombewa na mjumbe mmoja ambaye ni Mhe. Panya Ali Abdalla. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Wale wote wanaomuunga mkono Mhe. Panya Ali Abdalla kwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wanyanyue mikono, wanaomkataa, ameshinda kwa kura zote. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika, nafasi inayofuata ni nafasi ya Mweka Hazina wa UWAKUZA ambayo imegombewa na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf.

**Mhe. Spika:** Wale wote wanaomuunga mkono Mhe. Mtumwa Peya Yussuf wanyanyue mikono, wanaomkataa, ameshinda kwa kura zote. *(Makofi)*

**Katibu:** Mhe. Spika, nafasi ya mwisho ni nafasi ya Wajumbe wa Kamati Tendaji nayo imegombewa na Mhe. Habib Ali Mohamed na Mhe. Harusi Said Suleiman. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ni wajumbe wawili tu na wote wanatakiwa, ahsante naomba niwahoji kwa wote wawili wanaowaunga mkono wanyanyue mikono, wanaowakataa, Waheshimiwa wote wawili wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe naomba kabla sijamkaribisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwanza nitoe shukrani zangu za dhati sana. Katika mkutano huu tumekwenda vizuri sana, watu wenyeji hata wale wapya wamekuwa kama wapo siku nyingi sana humu ndani. Tunashukuru sana kazi zimefanyika vizuri.

Vile vile nina tangazo dogo, kwanza tangazo mara baada ya kuakhirishwa kwa kikao wanatakiwa Wajumbe wa CCM ambao sio mawaziri wakutane humu ndani kuna jambo muhimu ambalo Mnadhim wa Chama cha Mapinduzi anataka kuwapatia.

Baada ya tangazo hilo kwa heshima na taadhima sasa naomba nimkaribishe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ili aweze kuliakhirisha Baraza. Karibu sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

**KUAHIRISHA BARAZA**

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini la pili Mhe. Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema na mwenye kurehemu kwa kutujaalia uhai na kutupa afya njema na kutuwezesha kufanikisha Mkutano huu wa Pili wa Baraza la Kumi ulioanza tarehe 10/02/2021 na mategemeo ya kuakhirisha leo tarehe 25/02/2021. Mkutano huu ambao tumeweza kukamilisha shughuli zote zilizopangwa kwa mafanikio makubwa sana.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, familia ya marehemu na viongozi na wanachama wa Chama cha *ACT* Wazalendo na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kilichotokea tarehe 17/02/2021 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili Dar es Salaam na kuzikwa Wilaya ya Wete, Shehia ya Mtambwe, Pemba tarehe 18/02/2021. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. Amin.

Aidha, nawashukuru viongozi mbali mbali wa dini, vyama vya siasa, serikali na wananchi kwa kujitokeza kwa wingi katika mazishi na hitma zilizosomwa za kumuombea dua mpendwa wetu huyo Unguja na Pemba. Nawaomba wananchi tuendelee kushikamana na kushirikiana katika kuuendeleza umoja na amani ndani ya nchi yetu ili kumuenzi kiongozi wetu huyo aliyetangulia mbele ya haki.

Mhe. Spika, kwa niaba ya serikali nachukua nafasi hii kuwapongeza Wazanzibari wote na kuwashukuru kwa kujitokeza katika shughuli hii adhimu, ambayo ni shughuli ya lazima lakini kwa ushirikiano na mashirikiano makubwa bila ya tofauti ya aina yoyote. Mwenyezi Mungu atujaalie tuendelee kuimarisha ushirikiano wetu kwa mambo yote yatakayojitokeza ya furaha na msiba ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nampongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa na wananchi kwa asilimia 76. Vile vile, nampongeza Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa asilimia 84. Nawapongeza sana kwa uongozi wao mahiri na makini katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na serikali zetu. Kadhalika, nawapongeza wananchi kwa kushiriki kikamilifu katika mchakato

wa uchaguzi na kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuwachagua viongozi wanaowataka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuniamini na kuniteua kuwa Makamu wa Pili wa Rais, pia kumteua Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuwateua Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Wakuu na wateuliwa wengine wote ambao ndio watendaji wakuu wa shughuli za serikali. Aidha, kipekee kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa kwanza mwanamke Mhandisi Zena Ahmed Said, tokea kufanyika kwa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar 1964. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mkutano huu, Baraza lako tukufu limepokea miswada na ripoti mbali mbali kama zifuatazo:-

- Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2019/2020.
- Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara na Mashirika kwa mwaka 2018/2019.
- Ripoti ya Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar mwaka 2020.
- Hotuba ya Ufunguaji wa Baraza la Kumi la Wawakilishi aliyoitoa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 11/11/2020.
- Mjadala wa Mwelekeo wa Mpango wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 na Waraka wa Mpango wa Bajeti *(Budget Framework Paper).*
- Marekebisho ya Jadweli ya Pili ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar, Sheria Nam. 4 ya 2015.
- Kuwasilisha Barazani Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388*, "Revised Edition" (RE)* 2020 kwa mujibu wa Kifungu cha 132 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.
- Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbali Mbali; na
- Miswada kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, aidha katika mkutano huu Baraza lako limefanya chaguzi zifuatazo:-

- Uchaguzi wa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.
- Uchaguzi wa Wabunge watano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar.
- Uchaguzi wa Umoja wa Wanawake wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.
- Uchaguzi wa Viongozi wa Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola Kanda ya Zanzibar *(CPA).*

- Uchaguzi wa Chama cha Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumuiya ya Madola, Kanda ya Zanzibar *(CWP).*

- Uchaguzi wa Viongozi wa Umoja wa Wawakilishi wa Kupambana na Ukimwi Zanzibar (UWAKUZA).

Mhe. Spika, vile vile katika kikao hiki, Waheshimiwa Wajumbe walipata fursa ya kupatiwa mafunzo mbali mbali yaliyotolewa kwa njia ya warsha, semina zilizoandaliwa na Baraza kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali. Semina hizo ni kama zifuatazo:-

- Semina kuhusu masuala ya Kupambana na Rushwa na Mtandao wa Wabunge wa Kupambana na Rushwa Afrika *(APNAC).*
- Semina kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi.
- Semina kuhusu Protokali za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.
- Semina kuhusu Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola, Kanda ya Zanzibar *(CPA).*
- Semina kuhusu Chama cha Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumuiya ya Madola, Kanda ya Zanzibar *(CWP).*
- Semina kuhusu Umoja wa Wawakilishi wa Kupambana na Ukimwi Zanzibar (UWAKUZA).

Mhe. Spika, ni matumaini yangu kuwa mafunzo haya yataleta faida kubwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Mhe. Spika, katika mkutano huu jumla ya maswali ya msingi 91 na maswali ya nyongeza 201 yaliulizwa na yalijibiwa kwa ufasaha na ufafanuzi wa kina na Waheshimiwa Mawaziri. Hongereni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kuuliza maswali hayo na hongereni sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kujibu maswali hayo kwa uweledi mkubwa. Nyote mmetimiza majukumu yenu ya msingi ya kikatiba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali yetu imelenga kuinua hali za wananchi kiuchumi na kutatua kero mbali mbali zinazokwamisha harakati za maendeleo ndani ya nchi yetu.

Serikali inaendelea kuyatafutia ufumbuzi malalamiko na migogoro ya ardhi ambayo wananchi wengi hasa maskini wanakumbana nayo katika maeneo mbali mbali ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba. Hali hili inatokana na kuwepo kwa baadhi ya viongozi wanaojihusisha na vitendo hivi viovu. Hivyo, tunapenda kuwatahadharisha viongozi na watendaji wote wenye dhamana ya usimamizi wa ardhi kuacha mara moja, kwani serikali haitomvumilia mtu yeyote anayejihusisha na vitendo hivi na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Aidha, naiagiza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuharakisha utatuzi wa migogoro hiyo kwa haraka na kuchukuliwa hatua kali watendaji wote wanaohusika kwa namna moja ama nyengine katika migogoro hiyo, na kwa upande wa watendaji ambao hawapo kwenye mamlaka ya waziri tunaiagiza wizara ipeleke kwenye mamlaka inayohusika ili serikali ichukue hatua zinazohusika haraka iwezekenavyo.

Mhe. Spika, nchi yetu inaendelea kukumbwa na matukio ya udhalilishaji yakiwemo matukio ya ubakaji kwa wanawake na watoto, kupigwa, talaka zisizofuata utaratibu, kutelekezwa kwa watoto wachanga, ushirikishwaji kwa watoto katika biashara zikiwemo biashara haramu za dawa za kulevya. Kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kuwakumbusha wananchi wote kurudisha imani zetu kuanzia za kibinaadamu, kiutu, kijamii, kidini na kujenga umoja na mashirikiano kwa viongozi wa ngazi zote katika kupiga vita suala hili la udhalilishaji.

Aidha, serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa sheria na kuzifanyia marekebisho sheria hizo katika kukabiliana na janga hili. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uamuzi wake wa kuanzisha mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala la rushwa bado ni kero katika upatikanaji wa haki ndani ya taasisi na jamii zetu kwa jumla. Katika kuimarisha utawala bora, Serikali ya Awamu ya Nane imeamua kulivalia njuga suala hili ili kuhakikisha linaondoka ndani ya jamii zetu. Kwa kufanikisha hili serikali imeamua kuanzisha rasmi mahakama maalum kwa kesi zinazohusiana na rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato serikali imedhamiria kuongeza uwezo wa ukusanyaji mapato kwa kuchukua hatua madhubuti za kutanua wigo, kuelekea mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato yote ya serikali, kudhibiti mianya ya uvujishaji wa mapato, pamoja na kuwasisitiza wananchi kutoa na kudai risiti kila wanapouza na wanaponunua bidhaa au kupatiwa huduma. Sambamba na hili, serikali itahakikisha kwamba inasimamia vyema matumizi ya fedha za umma, kufuata taratibu na sheria zilizowekwa, pamoja na kuzingatia thamani halisi ya bidhaa au huduma kwa fedha inayotumika *(value for money)*.

Mhe. Spika, pato la nchi yetu linategemea sana sekta ya utalii, serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inasimamia na kuhakikisha kuwa Sekta ya Utalii inaimarika siku hadi siku. Hata hivyo, kumekuwa na tatizo la watalii wanaoingia nchini kupuuza na kutozingatia mila na silka za Kizanzibari na Kitanzania kwa ujumla, kuna baadhi ya watalii wamekuwa wakitembea mitaani bila ya kujistiri miili yao kama zinavyoelekeza tamaduni zetu. *(Makofi)*

Sambamba na hilo, pia kumekuwa na hali ya baadhi ya watalii kutofikia katika maeneo rasmi yaliyosajiliwa kwa shughuli za kitalii yakiwemo hoteli na nyumba za kufikia wageni na badala yake wamekuwa wakifikia katika maeneo yasiyo rasmi zikiwemo *"guest* bubu" hali hii inapoteza mapato yetu ya serikali.
Hivyo, ninaziagiza taasisi zote zinazohusiana na uingizaji na utembezaji wa watalii kutoa elimu kwa wageni juu ya kufuata mila, silka na tamaduni za Kizanzibari katika maeneo wanayotembelea. Pia, naziagiza taasisi zinazohusika na masuala ya kodi kufuatilia na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wale wote wanaokwenda kinyume na taratibu za nchi yetu juu ya suala hili la upotevu wa mapato yetu ndani ya nchi.

Mhe. Spika, serikali yetu imetanua wigo wa kiuchumi kwa kutilia mkazo suala zima la "Uchumi wa Buluu" ambao unahusisha sekta mbali mbali zikiwemo; utalii, uvuvi, kilimo, mafuta, gesi, michezo na usafiri. Kwa kuzingatia hili tayari serikali imeanza kuchukua hatua madhubuti ikiwemo kuunda wizara maalum inayoshughulikia sekta hii. Vile vile,

tumeshuhudia utiaji wa saini wa Hati ya Maelewano *(Memorandum of Understanding)* kwa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ya Mpigaduri na Bandari ya Mafuta na Gesi ya Mangapwani.

Nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kufanikisha hili ndani ya kipindi kifupi cha uongozi wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa upande wa huduma za kijamii, serikali itaendelea kuchukua hatua kila aina ya jitihada kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama, elimu, afya, makaazi bora pamoja na kuimarisha miundombinu kama inavyoelekeza katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025.

Serikali itaendelea kujenga majengo mapya ya skuli za msingi na sekondari pamoja na vituo vya Afya. Vile vile, serikali itafanyia ukarabati majengo yote yaliyochakaa, pamoja na kuimarisha miundombinu ya maji na barabara kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu.

Aidha, mbali na jitihada hizo serikali itaendelea kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunza katika skuli zetu, pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika hospitali na vituo vya afya vyote nchini.

Mhe. Spika, kwa kuimarisha uchumi wetu, serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi imedhamiria kuweka kipaumbele maalum ya uwekezaji kwa upande wa Kisiwa cha Pemba ili kuleta uwiano wa uwekezaji katika visiwa vyetu hivi viwili. Tutahakikisha kuwa tunaifanya Pemba kama ni eneo maalum la uwekezaji lenye vivutio vitakavyowavutia na kuwashajihisha wawekezaji kujitokeza kwa wingi kwa kuanzisha na kuendeleza miradi mikubwa ya kiuchumi kisiwani humo. Hatua hii itawezesha kuimarika kwa miundombinu ya kijamii na kiuchumi pamoja na kunyanyua hali za maisha ya wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, dunia inaendelea na mapambano dhidi ya maradhi ya *COVID-19* yanayosababishwa na virusi vya *Corona*, Zanzibar ni sehemu ya dunia; hivyo, nawaomba wananchi na Waheshimiwa Wajumbe kuendelea kushirikiana na wataalam wetu wa afya kuwasisitiza wananchi kufuata maelekezo na miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya, Ustawi Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto katika kujikinga na maradhi mbali mbali ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru tena na kukupongeza wewe binafsi, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wawili wote wa Baraza kwa kuviendesha vyema vikao vyetu kwa hekima, busara na uweledi mkubwa na kuufanya mkutano huu kuendelea na kumalizika kwa mafanikio makubwa. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kwa kutumia nafasi yao ya kidemokrasia ya kuisimamia, kuishauri na kuihoji serikali, jambo ambalo limeonesha nia thabiti mliyonayo ya kuitaka serikali kuwajibika ipasavyo kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Vile vile, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kujibu maswali yote waliyoulizwa, pamoja na kutoa ufafanuzi ambao uliwanufaisha Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa ujumla wanaotusikiliza. Halikadhalika, napenda kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufafanuzi wake alioutoa katika mambo mbali mbali yaliyohitaji ufafanuzi wa kisheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nawashukuru waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Pili wa Baraza la Kumi la Wawakilishi kwa uweledi na ufanisi mkubwa. Pongezi hizo zaidi ziwafikie Watendaji wote wa Baraza hili la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu, Ndugu Raya Issa Mselem. Pia nawapongeza wakalimani wa lugha ya alama ambao wamewawezesha wenzetu wenye mahitaji maalum ya huduma hiyo kuweza kufuatilia yote yaliyokuwa yakiendelea ndani ya Baraza hili Tukufu. Vile vile, nawashukuru wanahabari kwa kufanya kazi nzuri ya kuwapatia habari wananchi wetu kwa shughuli zote ambazo zilikuwa zikiendelea kufanyika. *(Makofi)*

Bila ya kusahau napenda nichukue fursa hii Mhe. Spika, kuwapongeza sana wapenzi, watani wetu wale wa *Simba Sports Club* kwa ushindi mdogo sana walioupata juzi, lakini ni ushindi muhimu na sisi kama wanamichezo tunawapongeza sana. Nilimsikia pale Mhe. Machano Othman Said kwamba aliwapongeza wapenzi wa Yanga walikwenda kumuangalia, wapenzi wa Yanga ni kawaida yao hata tunaowatibu viongozi wa Simba. Mhe. Spika, ile ni timu ya wananchi kwa hiyo, kila mwananchi anatibiwa tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kwa heshima na taadhima kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liakhirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 05 Mei, 2021 saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante waheshimiwa hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wote ambao wanaunga mkono hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Waheshimiwa Wajumbe, mimi nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake lakini na utani huu wa dakika ya mwisho ambao umewachangamsha sana humu Waheshimiwa Wajumbe. Kabla sijaakhirisha waheshimiwa ninalo tangazo jengine, hili tangazo limeletwa na Mhe. Hamza Hassan Juma sio kwa nafasi ile ya Unadhim kwa nafasi nyengine kabisa, ambapo anaomba kuwatangazia wajumbe kuwa msiondoke maana kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa michezo wa *Baraza la Wawakilishi Sports Club.* Kwa hiyo, alikuwa anawaomba wajumbe wabaki ili uweze kufanyika huo uchaguzi wa viongozi kwa sababu huo sasa unafanyika nje ya Baraza kwa maana nje ya shughuli hizi za Baraza za kwenye *order paper. (Makofi)*

Baada ya tangazo hilo Waheshimiwa Wajumbe naomba sote sasa tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

**WIMBO WA TAIFA**

Ahsante Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hapo sasa, naomba niakhirishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatano tarehe 05 Mei, 2021 saa 3:00 barabara za asubuhi.

*(Saa 5:24 asubuhi Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 05/05/2021 saa 3:00 asubuhi)*